*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 27 Mei, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Daudi Protas Venant.

Na. 273

**Uhitaji wa Ujenzi wa Daraja Katika Mto Loya**

**MHE. VENANT D. PROTAS** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja katika Mto Loya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Igalula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TARURA* katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 imetenga shilingi milioni 318.90 kwa ajili ya usanifu wa daraja la Mto Loya ambapo tayari kazi ya usanifu ilianza tarehe 22 Desemba, 2021 na inategemea kukamilika tarehe 21 Juni, 2022 ambapo gharama halisi za ujenzi zitakuwa zimejulikana. Kazi hiyo ya usanifu inafanywa na Mhandisi Mshauri *Advanced Engineering Solutions* ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujulikana kwa gharama za ujenzi huo ambao unalenga kujenga daraja kubwa na daraja la watembea kwa Miguu ikiwa ni pamoja na kujenga barabara *approach road* yenye urefu wa

kilometa 13, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Venant.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nikiri wazi kweli wataalam wako katika Kata ya Loya, wanafanya usanifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maswali yangu mawili ya nyongeza la kwanza, tarehe 17 Mei, Mheshimiwa Rais alipokuwa Mkoa wa Tabora nilimfikishia kero hii ya wananchi wa Loya na akamuagiza Waziri wa Ujenzi aweze kushughulikia daraja hilo.

Je, Serikali kupitia Wizara ya TAMISEMI, hamuoni kuharakisha huo usanifu ili mpeleke Wizara ya Ujenzi ili muweze kusaidia kujenga daraja hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili, kwa kuwa daraja hili litachukua muda mrefu kukamilika na wananchi wanaendelea kupoteza maisha, hamuwezi kuona uharaka kwa kujenga daraja la watembea kwa miguu ili wananchi wasiendelee kupoteza maisha? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Igalula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho nina uhakika nacho ni kwamba tuko katika hatua za mwisho za kukamilisha usanifu ambao mpaka sasa hivi tumebakiza kama wiki tatu tu kukamilika. Kwa hiyo, mara baada ya kukamilika basi tutakabidhi kwa wataalam kwa ajili ya hizo fedha ili sasa zipatikane na ujenzi wa daraja uanze. Kwa hiyo, uharaka wa

kujenga daraja la miguu kwa sababu hizi kazi zinaenda sambamba, nimhakikishie tu kwamba tutafanya haya yote kwa pamoja kuhakikisha kwamba wananchi wale wanapata huduma, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona daraja la Zihi – Mlambalasi kwenda Kiwele ambalo ni Jimbo la Kalenga ni daraja ambalo ni muhimu sana linatakiwa lijengwe kwa sababu linakwenda kwenye makumbusho ya Mkwawa.

Ni lini Serikali italijenga daraja hilo kwa sababu sasa hivi watu wanapita tu, ni kasehemu kadogo wanapita kwa pikipiki tu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Grace Tendega, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunajenga madaraja ambayo yamekuwa sumbufu katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa hiyo, niwaagize tu Mkandarasi wa *TARURA* Mkoa wa Iringa waweze kwenda kufanya tathmini na baada ya tathmini tutafute fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, Mto Bubu umekata katikati kati ya Kijiji cha Mpendo - Hamia na hivyo kipindi cha mvua kuna na ugumu sana wa kupata mawasiliano ya barabara kuja Dodoma. Nini mkakati wa Serikali walau wa kujenga daraja la muda ili watu wapate mawasiliano? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Monni, Mbunge wa Chemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tumelipokea ombi la Mheshimiwa Mbunge na tutatuma wataalam wetu waende wakafanye tathmnini waone ni namna gani linaweza likatekelezeka ndani ya muda mfupi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Mafuwe.

Na. 275

**Ahadi ya Ujenzi wa Soko la Kisasa la Kwasadala – Hai**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa soko la kisasa la Kwa Sadala?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Hai imeandaa andiko la mradi wa ujenzi wa soko la Kwa Sadala wenye thamani ya shilingi bilioni tisa. Andiko hilo limefanyiwa uchambuzi na Mkoa ambapo mapungufu yaliyojitokeza yamewasilishwa Halmashauri kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pindi marekebisho hayo, yatakapokamilika na kukidhi vigezo Serikali itatafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa taarifa ambazo nimepewa taarifa hii na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, ni kwamba tayari marekebisho yao yameshafanyika na imeshawasilishwa kwenye mamlaka ya ofisi yake. Swali langu, itakapofika kwenye meza yako, ni lini Serikali itaanza ujenzi huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa soko hili likikamilika litahitaji sana mizigo mingi kutoka pembezoni kwenye maeneo mbalimbali na kata mbalimbali. Serikali ina mpango gani sasa wa kutekeleza ahadi ya Rais kwa kujenga barabara ya Shilinjoro - Mijengweni, *Arusha Road* – Ngalawa; na barabara ya Jiweni – Lukan - Losaa - Nakyungu? ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Hai ambayo tulikuwa tumeiadikia kufanya marekebisho, wapo kwenye hatua na kwa maelezo ya Mheshimiwa Mbunge ni kama wamekabidhi.

Ninachoweza kumhakikishia ni kwamba Serikali ya Awamu ya Sita, itakapopata andiko hilo maana yake tutaanza mara moja kutafuta fedha ili sasa tutekeleze ahadi ambayo ipo ya kujenga soko hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya kukamilika kwa soko maana yake tutafuta fedha zaidi sasa kurekebisho hizo barabara ambazo zinaelekea katika eneo la soko ili kurahisisha uchumi wa wananchi wa Hai. Kwa hiyo, hicho ndicho nachoweza kusema ahadi ya Serikali ya Awamu ya Sita.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Regina Ndege.

Na. 274

**Kuongeza Kiwango cha Mkopo wa Halmashauri Unaotolewa kwa Vikundi vya Watu Watano**

**MHE. REGINA N. QWARAY** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuongeza kiwango cha mikopo ya vikundi vya watu watano inayotolewa na Halmashauri kutoka shilingi milioni moja hadi shilingi milioni tano?

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 9 ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2019 imeelekeza kwamba fedha za mikopo zitakazotolewa zitatumika kwa miradi iliyoidhinishwa na Kamati ya Kudumu ya Fedha, Mipango na Uongozi kwa kuzingatia ushauri na mapendekezo ya Timu ya Menejimenti na Kamati ya Huduma za Mikopo. Hivyo, ni jukumu la kikundi husika kuomba mkopo kulingana na mahitaji ya mradi husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Regina.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kwa fedha hizi ni *revolving funds* lakini bahati mbaya sana baadhi ya vikundi vinashindwa kufanya mrejesho. Je, Serikali inawachukulia hatua gani vikundi ambavyo vinashindwa kufanya mrejesho ili vikundi vingine vipate mikopo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa biashara nyingi zilizoanzishwa na vikundi hivi vina-*fail.* Je, Serikali haioni haja sasa ya kufanya uchambuzi wa kina na ushauri kabla hawajatoa mikopo katika vikundi hivyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba wale wote ambao hawalipi mikopo kuna hatua ambazo zimekuwa zikichukuliwa katika kila Halmashauri, ikiwemo kuwafuata, kuwaelimisha, lakini vilevile wale ambao wamekuwa wagumu kesi zao za madai zimekuwa zikipelekwa mpaka mahakamani na wengine wamekuwa wakilipa. Kwa hiyo, tunaandaa mpango ambao utafanya sasa watu wote wanaokopa waweze kulipa kwa wakati ili fedha zile ziwasaidie na watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, tumepokea ushauri na sasa hivi tunajaribisha kuwapa elimu Maafisa Maendeleo wa Jamii ili waweze kufanya uchamuzi wa kina pamoja na ushauri sahihi wa wale wote wanaokop ili mikopo hii iwe na tija. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyamonga.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, kwa kuwa mikopo hii mara inapotolewa wakopaji uanza kulipa mara moja, lakini wapo wakulima wa mazao ya muda mrefu kama parachichi na mazao mengine yanayochukua muda mrefu. Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa kipindi cha kusubiria yaani *grace period* kabla hawajaanza? Uko tayari kutoa agizo hilo Mheshimiwa Naibu Waziri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nyamoga, Mbunge wa Jimbo la Kilolo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo hii inaongozwa kwa kanuni na sheria iliyotungwa na Bunge. Kwa hiyo, mpaka muda huu ninapozungumza bado kanuni zinazotumika ni zile ambazo zimetungwa. Kwa hiyo, ili kuongeza *grace period* maana yake tunahitaji mabadiliko ya kisheria ili tuweze ku-*accomadate.* Kwa hiyo, Bunge lako tukufu litakavyoona wakati unafaa basi mnaweza kufanya marekebisho na sisi tutatekeleza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Sima.

Na. 276

**Changamoto ya Utekelezaji wa Sera ya Elimu Bila Malipo**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA K.n.y MHE. MUSSA R. SIMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na changamoto ya uhaba wa walimu, madarasa, samani na

miundombinu mingine inayochagizwa na utekelezaji wa Sera ya Elimu bila Malipo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Mbunge wa Singida Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua kukabiliana na upungufu wa walimu katika shule za msingi na sekondari nchini kwa kuajiri walimu na kuwapanga katika maeneo yenye uhaba, kufanya msawazo wa walimu katika maeneo yasiyo na walimu wa kutosha

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika kukabiliana na changamoto ya miundombinu ya elimu inaendelea kujenga shule mpya, madarasa yenye samani ndani yake na kuboresha miundombinu chakavu kupitia bajeti ya Serikali na miradi ya kuboresha elimu kama vile *BOOST, SEQUIP, EP4R* na *GPE LANES II.*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, katika Jimbo la Manyoni Mashariki kuna Kata ya Makutupora ambayo ilipangiwa kujenga shule mpya, lakini mpaka sasa hivi fedha ya kujenga shule mpya katika Kata ya Makutupora haijapelekwa. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka fedha hii ili shule ianze kujengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa utoaji wa elimu ya awali katika Mkoa wa Singida bado ni hafifu; je,

nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba sasa tunaajiri walimu wa elimu ya awali hususani katika maeneo ya vijijini ya Mkoa wa Singida? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Chaya, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Mashariki kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi ya Serikali na ujenzi wa shule ya sekondari katika Kata ya Makutupora iko pale pale na tutajenga kata hiyo kwa sababu fedha zipo katika bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili kuajiri walimu wa awali katika ajira hizi zilizotangazwa moja ya kigezo ambacho tumezingatia ni kuajiri walimu wapya ambao wana shahada ya elimu ya awali na stashahada ambao tutawapeleka katika shule zote nchini ili kusaidia hii elimu ya awali nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na uhaba mkubwa wa watumishi katika Wilaya ya Liwale, lakini hata hivyo mgao tunapata watumishi, lakini idadi ya watumishi wanaohama na wanaohamia kubwa ni ile ambayo wanahama bila kufanyiwa *replacement.*

Je, nini kauli ya Serikali juu ya kuhamisha watumishi bila kutupatia *replacement* kuziba nafasi hizo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Jimbo la Liwale, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunatambua changamoto za maeneo ya pembezoni walimu wengi wanaoajiriwa huwa wanapenda kuhama na sasa hivi mkakati wa Serikali ni kwamba watu wote ambao tunawaajiri tunawapa na ile barua kwa maana ya *commitment letter* ambayo itawafanya wakae maeneo siyo chini ya miaka mitatu mpaka watakavyoomba kuhama. Lengo la Serikali ni kuhakikisha maeneo yote nchini yanakuwa na usawa wa walimu wote ambao tunawaajiri, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Omar Issa Kombo.

Na. 277

**Kukifanyia Ukarabati Kituo cha Polisi Micheweni**

**MHE. OMAR ISSA KOMBO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakifanyia matengenezo Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Micheweni na ujenzi wa nyumba za askari?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya tathmini ya uchakavu wa Kituo cha Polisi Micheweni na kubaini kuwa kiasi cha fedha shilingi 51,000,000 zinahitajika kwa ajili ya

ukarabati wa kituo hicho. Aidha, ujenzi wa jengo la hanga la kituo hicho umefikia kwenye hatua za kumalizia na kiasi cha fedha shilingi 57,000,000 zinahitajika. Ukarabati wa kituo pamoja na umaliziaji wa ujenzi wa jengo la hanga utafanyika kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kombo.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali ingawa hayaleti matumaini kwa wananchi wa Wilaya ya Micheweni, lakini nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na hali ya kituo kilivyo hali ni mbaya sana mpaka paa zake kuvunja. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka na wa dharura kukarabati Kituo hiki cha Micheweni?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari baada ya Bunge hili kuambatana na mimi mpaka Micheweni kwenda kujionea hali halisi ilivyo kwa sababu hanga hili la polisi limejengwa kwa nguvu za wananchi takribani miaka minane iliyopita na sasa hivi tayari limeanza kuvuja. Je, uko tayari kuambatana na mimi kwenda kujionea hali halisi ilivyo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kombo kama ifuatavyo:-

Kwanza nakubaliana naye kwamba hali ni mbaya ndiyo maana tathmini yetu imefanyika na kubaini gharama zinazohitajika.

Kwa kuwa bajeti ya mwaka huu imepita, naomba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba katika maeneo yatakayopewa vipaumbele katika mwaka ujao basi tutazingatia hili eneo pia la Micheweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umuhimu wa kuambatana naye niko tayari na mara nyingi natekeleza ahadi baada ya Bunge hili tutapanga tuone lini kuweza kuitembelea Micheweni kubaini kiwango cha uharibifu na nakubaliana naye pamoja namna ya kutekeleza ukarabati huo, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakagenda

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi cha Tukuyu hakina uzio kwa ajili ya usalama wa kituo kile kwa sababu inazungukwa pia na shule ya msingi. Ni lini Serikali itapeleka pesa katika kituo kile ili tuweze kujengewa uzio kwa usalama wa wananchi wanaozunguka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kupanga ni kuchagua, tumesema sasa hivi baadhi ya vituo ni chakavu sana, vinahitaji ukarabati na kwingine kunahitaji kujenga kabisa. Kwa hiyo, swali la Mbunge ni zuri kweli tunahitaji uzio, lakini kwa vipaumbele tulivyoweka uzio itakuwa ni *second priority* tutaanza kwanza na ukarabati hatimaye uzio utafuata, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa...

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante Kituo cha Polisi Mbogwe...

**NAIBU SPIKA:** Ngoja ngoja Leonard Maganga?

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Nicodemas Maganga.

**NAIBU SPIKA:** Maana leo umependeza, sijakutambua vizuri. *(Makofi)*

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi Masumbwe kiko kwenye eneo la CCM na tumeshachukua eneo kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi pale Mbogwe.

Je, Serikali inatusaidiaje Mbogwe ili kusudi askari wapate mahala pa kukaa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mbunge kwa mahusiano mema na Chama Tawala, Chama cha Mapinduzi ambao waliweza kutoa jengo linalotumika na Kituo hicho cha Polisi. Hata hivyo kama tulivyokwishasema kwenye majibu yetu ya msingi mbalimbali ni kwamba kipaumbele ni kujenga vituo vya polisi kwenye maeneo ambayo hayana kabisa, Mbogwe ikiwa ni mojawapo tutaipa kipaumbele katika miaka ijayo ili kuweza kujengea kituo chake cha polisi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri katika majibu yako umeandika; "...hatua ya kumaliza na kiasi cha fedha shilingi milioni 57 zinahitajika. Ukarabati wa kituo pamoja na umalizaji wa ujenzi wa jengo la hanga utafanyika kulingana na upatikanaji wa fedha." Hili si jibu sahihi la Kibunge. Jibu sahihi linatakiwa utafanyika kulingana na ratiba iliyopangwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Kidogo haileti sura nzuri.

Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mheshimiwa Stella Manyanya.

Na. 278

**Rasilimali za Kiwanda cha *Mang'ula Mechanical and Machine Tools* Kutumika kutoa Mafunzo ya Ufundi**

**MHE. ENG STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Je, ni kwa nini Serikali isitoe rasilimali za Kiwanda cha *Mang'ula Mechanical and Machine Tools* kilichopo Kilombero kwa Taasisi za Ufundi kama *DIT* na nyinginezo ili ziweze kutumia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA,** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Jimbo la Nyasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeamua kukihuisha upya kiwanda cha *Mang'ula Mechanical & Machine Tools Co. Ltd.* kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* ili kiendelee kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa hapo awali. Ikiwa kutakuwa na haja ya kuzihusisha Taasisi za Ufundi Serikali itafanya hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Uzoefu unaonesha kwamba taasisi nyingi ambazo ziko chini ya *NDC* hazifanyi vizuri kutokana na ukosefu wa fedha kwa mfano *General Tyre*, *Kilimanjaro Machine Tools* na kadhalika.

Swali langu katika bajeti ya mwaka huu 2022/2023 Wizara imeanza kutenga fedha zozote kwa ajili ya kuendeleza kiwanda hicho cha *Mang'ula Machine Tools*?

Kwa kuwa kiwanda kile kimenyofolewa maeneo muhimu karibu yote kwa mfano sehemu za *foundry* imenyofolewa kiasi kwamba ni ngumu kukirudishia kama kilivyo na kitahitaji gharama kubwa sana. Kwa nini kwa sababu kuna majengo ambayo yanawezesha kukaa wanafunzi eneo hilo lisitumike kwa ajili ya kuendeleza taasisi za kiufundi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stella Manyanya, Mbunge kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Stella Manyanya kwa kazi kubwa anayoifanya kufuatilia maendeleo ya sekta ya viwanda kwa sababu na yeye amekuwepo kwenye sekta hiyo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni kweli Shirika letu la Maendeleo la Taifa *(NDC)* lina miradi mingi ambayo kidogo ina changamoto lakini tumeshaanza kuyafanyia kazi ikiwemo *Kilimanjaro Machine Tools* ambako tumepeleka fedha ya kutosha kwa ajili ya kuihuisha ili kutengeneza *foundry* ambayo inafanana fanana na ile iliyokuwepo kule Mang'ula.

Kwa hiyo tumeshaanza kutengea fedha, lakini kwenye hii mahsusi ya Mang'ula baada ya kuona uhitaji huu tunafanya utafiti wa kuona nini kitafanyika halafu baada ya hapo sasa ndiyo tutakuja na bajeti yenye uhalisia. Kwa hiyo, tuko kwenye hatua za awali za kufanya utafiti wa nini kitafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu mitambo iliyokuwepo ni kweli na ndiyo maana tunataka tukihuishe kwa maana tuone sasa nini kitafanyika kwa sababu mwekezaji aliyekuwa amepewa mara ya kwanza ni kweli aling'oa mitambo mingi ikiwemo ya *foundry*, ya *forging* na *fabrication* na kuuza. Kwa hiyo, kimsingi tutaanza kama upya lakini kwa

sababu nia ya Serikali nia ya kuona tunahuisha viwanda hivi kwa hiyo Serikali imeweka mkazo na tutakifanyia kazi na kutenga bajeti ya kutosha ili tuhakikishe tunarudi kwenye uhalisia wake wa awali, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Maji Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi.

Na. 279

**Hitaji la Maji Tarafa ya Mtae – Lushoto**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italishughulikia tatizo la maji kwa vijiji zaidi ya 14 vya Tarafa ya Mtae?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa ya Mtae ina jumla ya vijiji 20 ambapo vijiji 16 vinapata huduma ya maji kupitia visima vifupi na mito. Katika kuboresha huduma hiyo, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imekamilisha ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji ya Bokoboko, Shaghayu na Rangwi inayonufaisha vijiji sita vya Masereka, Mamboleo, Kwemtindi, Tema, Mpondekaya na Kweshindo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, Mradi wa Rangwi ambao ameutaja hapa ambao una vijiji karibia vinne vya Goka, Nhelei, Kalumele na Mamboleo ni mradi ambao sasa umechakaa, lakini pia eneo la usambazaji limekuwa dogo kwa sababu idadi ya watu imeongezeka. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuboresha mradi huo?

Pili, katika kata ya Sunga, Tarafa hiyo hiyo ya Mtae vijiji vyote vinne havijawahi kuwa na mradi wowote wa mfumo wa maji ya bomba. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka na kata hii ya Sunga iweze kupatiwa miundombinu ya maji safi ya bomba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shangazi kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunafahamu mradi ule umechakaa na kama Wizara tayari tumeuweka kwenye mpango wa mwaka 2022/2023 ili kuona kwamba tunakwenda kukarabati na kuweza kuwafikishia wananchi wote wa maeneo aliyoyataja maji mengi, safi, salama na ya kutosha.

Swali lake la pili anaulizia kuhusu Kata ya Sunga ambayo ina vijiji vinne ni kweli mtambao wa mabomba kwenye kata hii haukuweza kufikiwa kulingana na jiografia ya eneo lenyewe. Vyanzo ni kweli viko vingi katika eneo lile, lakini vyanzo vingi viko maeneo ya chini na wananchi vijiji viko kwenye miinuko kwa maana kwenye milima hivi kidogo kama tunavyofahamu jiografia ya Lushoto lakini kama Wizara tunaendelea kuona uwezekano wa kupata vyanzo vya kujitosheleza maeneo yale ya juu na hatimaye kabla ya mwaka ujao wa fedha tutahakikisha tunapata na kuweza kuwafikishia maji ya bombani wananchi wote wa Kata ya Sunga yenye vijiji vinne.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kitandula .

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naomba niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mji wa Kasera ambayo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga bwawa lake linalopeleka maji hapo linakaribia kukauka, tumeleta maombi ya dharura takriban shilingi milioni 51. Je, ni lini fedha hizi zitapatikana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kitandula, Mbunge wa Mkinga kama ifuatavyo. Tunatarajia wiki ijayo kuwapelekea shilingi milioni 51 kwa ajili ya bwawa hilo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Twaha jiandae Dkt. Musukuma, jiandae Mheshimiwa Midimu.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo la Kibiti kata ya Mtawanya kuna vijiji vya Bumba, Msola na Makima vina shida kubwa sana ya maji.

Ni nini tamko la Serikali kuhusiana na kuweka maji katika maeneo hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Twaha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kata hii anayoiongelea tumeshazungumza mara kadhaa na Mheshimiwa Mbunge na tayari tunaiweka kwenye utaratibu wa kuona kwamba tunawaletea wananchi maji bombani yakiwa safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ningependa kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri mradi wa miji 24 ni mradi ambao ulikuwa ni mkombozi sana kwenye Mji wa Geita ambapo Jimbo la Geita Vijijini kata tano zilikuwa zinafaidika Senga, Kagu, Nyawilimilwa, Bugurura na Kakubiro. Lakini tumekuwa tukiahidiwa kila siku hatuoni mwelekeo; je, ni lini Serikali itaanza sasa kutekeleza mradi huo wa miji 24?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Musukuma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa NaibU Spika, kwanza niseme siyo vijiji mini 24 bali ni miji 28, lakini vile vile Geita Mjini kata hizo tatu zinakwenda kunufaika hivi punde subira yavuta heri. Maandalizi yote yamekamilika tunasubiri tu kusaini, tunasubiri na muda na nafasi ya Mheshimiwa Rais.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itaboresha usambazaji wa mabomba ya maji katika Kata ya Bariadi, Mtaa wa Kidinda, Majengo Viwandani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usambazaji wa maji katika mji wa Bariadi kwenye maeneo aliyoyataja ni moja ya maeneo ambayo tumeyapa jicho la kipekee kuhakikisha

tunakwenda kuyafikia lengo ni kumtua mwanamama ndoo kichwani na kusambaza maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Noah Saputu.

Na. 280

**Mradi wa Maji wa Vijiji Tisa - Arumeru Magharibi**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga mradi wa maji wa vijiji tisa vya Kata za Oldonyosambu na Oldonyowas?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mradi wa maji wa Oldonyosambu kwa ajili ya kuhudumia vijiji tisa vya kata za Oldonyosambu na Oldonyowas. Utekelezaji wa mradi huo unahusisha ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 47.8, ujenzi wa matanki matatu yenye ujazo wa lita 575,000, ujenzi wa vituo vitatu vya kuchotea maji na *booster stations* mbili. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2022 na kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji katika kata hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saputu.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimia Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa mradi huo umechukua muda mrefu na sasa wananchi wanakunywa maji ya *floride* na wanazaliwa watoto wenye vichwa vikubwa, vibiongo na miguu kupinda. Je, Serikali haioni sasa kufanya haraka kwa ajili ya kukamilisha mradi huo?

Swali la pili, je, Naibu Waziri wa Maji baada ya Bunge hili atakuwa tayari kwenda kukagua mradi huo ili kujionea hali halisi ya wale wananchi wanavyoteseka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Saputu kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mradi tumeweka nguvu kubwa lakini tumekusikia Mheshimiwa Mbunge tutaongeza nguvu.

Swali la pili kukagua mradi mara baada ya Bunge hili Mheshimiwa Mbunge unafahamu nilishakuja Jimboni kwako hivyo sitasita kufika tena kuhakikisha huduma ya maji inapatikana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru; Mheshimiwa Waziri *Engineer* rafiki yangu nadhani wananchi wa Nyatwali nilikukutanisha nao kata yao wana mradi mkubwa umekamilika na wamekuambia huo mradi haujazinduliwa, kigugumizi cha kuzindua huo mradi ni kitu gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya kama ifuatavyo:-

Ni kweli Mheshimiwa Ester tulikutana na wale madiwani na wananchi wa ile kata nilikubali nitakuja tusubiri Bunge liishe tutafika na litazinduliwa kwa sababu tunahitaji wananchi wapate maji.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mtenga.

Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji kwa majibu sahihi.

Na. 281

### Kutoa Fedha kwa Ajili ya Jengo la Abiria Uwanja wa Ndege Mtwara

**MHE. HASSAN S. MTENGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la abiria katika uwanja wa ndege Mtwara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo la abiria katika kiwanja cha ndege cha Mtwara litajengwa katika awamu ya pili ya ukarabati na upanuzi wa kiwanja hicho. Hivyo, fedha itatolewa baada ya kukamilika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Mradi huu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtenga.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa uwanja wa Mtwara inawezekana tukauita *international airport* kwa sasa *package* yake ya mradi ule ulikuwa ni kuwepo na gari ya zimamoto nikimaanisha *fire*. Je, ni lini sasa Wizara itahakikisha kwamba mkandarasi anatuletea gari ya zimamoto pale *airport*?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili uwanja wa *airport* umepakana na maeneo ya wananchi, lakini baadhi ya maeneo ya wananchi lilipita bomba la gesi na wananchi wale wakalipwa. Sasa ni lini Serikali itaamua kuwalipa wananchi ambao bado hawajalipwa ili waondokane na adha hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtenga hilo swali tofauti na swali la msingi, jibu la kwanza tu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini kama ifuatavyo:-

Naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika ukarabati na upanuzi wa uwanja huu suala la gari la zimamoto ni sehemu ya mradi huu na tayari mkandarasi ameshatoa *order* gari itanunuliwa kutoka Ujerumani na thamani yake itakuwa ni bilioni 1.4. Kwa hiyo tayari gari limeshaanza kutengenezwa kwa ajilli ya uwanja wa Mtwara, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Norah Mzeru.

Na. 282

## Ujenzi wa Barabara ya Morogoro – Malinyi – Namtumbo kwa Kiwango cha Lami

**MHE. NORAH W. MZERU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Morogoro – Malinyi – Namtumbo kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutafuata fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Ifakara – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo - Londo hadi Lumecha (Namtumbo) kwa kiwango cha lami. Kwa sasa maeneo yote korofi yataainishwa na kujengwa ili barabara hii ipitike mwaka wote, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Norah.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante ni upi sasa mkakati wa Serikali wa kujenga barabara zote za Morogoro ili ziweze kupitika msimu mzima?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE).** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba baabara zote za Mkoa wa Morogoro zinapitika ni pamoja na kuzijenga zile ambazo tumeziainisha kwa kiwango cha lami, lakini pia kuzitengea fedha barabara zote kwa ajili ya ukarabati na kuna barabara ambazo tayari zipo kwenye kutangazwa kwa ajili ya kuzijenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba azma ya Serikali ni kuhakikisha barabara zote zinapitika mwaka mzima, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia ametangaza kwa nguvu kubwa utalii kupitia *Royal Tour* na kwa kuwa barabara zinazokwenda katika Mbuga za Wanyama kama *Ruaha National Park* hadi leo hazijajengwa kwa kiwango cha lami.

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba barabara zote zinazokwenda katika mbuga za wanyama zinajengwa kwa kiwango cha lami ili watalii watakapokuja tutendewe haki na Nyanda za Juu Kusini tupate watalii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Iringa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa kuanza na barabara ya Iringa kwenda *Ruaha National Park,* Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara hiyo, lakini pia Benki ya Dunia *(World Bank)* imeonesha nia ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa maana ya barabara zote zinazoenda kwenye mbuga kama ukipitia kwenye kitabu chetu cha bajeti barabara nyingi zinazokwenda kwenye mbuga zimefikiriwa na kutengewa fedha ili kuboresha sekta hii ya utalii ambayo Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan tumeona jinsi ambavyo amefanya kwenye *Royal Tour* kwa hiyo na sisi hatutamwangusha kuhakikisha kwamba tunatengeneza miundombinu bora kwa

ajili ya watalii kwenda kwenye mbunga za wanyama, ahsante

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Butondo, jiandae Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kuuliza ni lini barabara ya Kolandoto kwenda Mwangongo yenye kilometa 63 itaanza utekelezaji kwasababu mwaka huu wa fedha imetengewa bajeti ya fedha shilingi 2,000,000,000? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Butondo, Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii tumeiweka kwenye mpango kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango la lami kuanzia Kolandoto hadi Lalago na Lalago hadi Mwanuzi kilometa hizi 62 na kilometa 60 katika mwaka huu wa fedha, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara ya kutokea Namtumbo kwa maana ya Lumecha, Kitanda, Londo, Malinyi, Kilosa kwa Mpepo hadi Lupilo wakati Mheshimiwa Waziri anajibu hoja za Wabunge kwenye hotuba yake alisema imeingizwa au imeorodheshwa katika mpango wa *EPC, something like that* ambao utahusisha wajenzi binafsi.

Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza ukawaeleza vizuri wananchi wa maeneo hayo hususani wananchi wa Namtumbo na Malinyi kwa sababu hawakuelewa vizuri mpango huu ukoje ili wajue barabara hii itajengwa na mpango huu lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye jibu langu la msingi kwanza tutakuwa na mpango wa muda mfupi kuhakikisha kwamba tunaainisha maeneo muhimu korofi tuweze kuyakarabati ili barabara hii ipitike kwa muda wote, lakini kwa suala la *EPC+F* kwa maana ya *Engineering Procurement Construction and Financing,* ni suala ambalo litahitaji muda. Nitamuomba Mheshimiwa Vita Kawawa kama ataweza akatuletea swali la msingi ama tutakutana naye ili kuweza kulielezea kwa mapana na marefu kwa ajili ya kutoa uelewa kwa Waheshimiwa Wabunge wote, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri Mheshimiwa Waziri hongera sana ahsante. Maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni waliopo Jukwaa la Spika wageni 31 wa Bunge ambao ni Waandishi wa Habari Wanawake kutoka Mikoa mbalimbali Tanzania, wakiongozwa na Ndugu Joyce Mwakilinga, naomba msimame kwa pamoja, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Bunge ambao ni washindi wa *Miss Tanzania* namba moja hadi namba tatu na wafadhili wao kutoka jijini Dar es Salaam Ndugu Halima Ahmed Kopwe; *Miss Tanzania* simameni kwa pamoja. *(Makofi)*

Sasa yule *Miss Tanzania* asimame peke yake tumuone na hasa nguo hiyo ndiyo imekubeba sana hiyo. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge wapo wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge waliotembelea Bunge wasimame kwa pamoja wageni wote wa

Waheshimiwa Wabunge simameni wote kwa pamoja tafadhali, ahsanteni karibuni, pamoja na yule msanii kutoka Mtwara na Lindi *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 68 na walimu watatu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Regina Mundi ya Ulanga, Morogoro, karibuni sana, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wanafunzi 28 wa Shahada ya Uzamili katika Utawala na Usimamizi wa Elimu kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM),* hongereni na karibuni. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anawatangazia Wabunge kwamba siku ya Jumatatu tarehe 30 Mei, 2022 saa 7.00 mchana kutakuwa na semina kwa Wabunge wote itakayohusu maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022. Semina hiyo itaendeshwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na itafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa, Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa kuhudhuria semina hiyo muhimu sana.

Katibu anaendelea kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira inawaalika Wabunge wote kushiriki katika Maadhimisho ya Wiki ya Mazingira yatakayofanyika kuanzia tarehe 28 Mei hadi tarehe 5 Juni, 2022 ambapo kitaifa yatafanyika katika Jiji la Dodoma, shughuli zilizofanyika ni pamoja na tarehe 28 Mei, 2022 ni siku ya uzinduzi ambayo kuanzia saa 12.30 asubuhi yatafanyika matembezi ya hiyari yatakayoanzia maeneo ya Bunge hadi makutano ya barabara ya Dar es Salaam na barabara inayoelekea kwa Waziri Mkuu na kufuatiwa na shughuli ya upandaji miti, mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Tarehe 5 Juni, 2022 ni siku ya kilele cha maadhimisho ya siku ya Mazingira Duniani yatakayofanyika kuanzia saa 2.30 asubuhi katika ukumbi wa Mkutano wa Jakaya Kikwete

Jijini Dodoma na Mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa sana kuhudhuria sherehe hizo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jana nilimuona Mheshimiwa Rose Tweve ndani kwenye Bunge humu na kwa kweli lazima niwapongeze kwa Wabunge wawili kuoana humu ndani ni neema kwetu. *(Makofi)*

Na kwa kweli sidhani kama hata nyie mligundua kama kulikuwa na vitu vinapita pita, lakini wamefanya heshima na wamefanya staha mpaka kufikia kuunganisha roho zao pamoja. Kwa hiyo, mimi nawapongeza sana. *(Makofi)*

Na mke usioe mke mzuri, oa mke mwema kwa sababu uzuri unakwisha, wema hauishi na usioane na mwanaume mzuri, oana na mwanaume mwema kwa sababu uzuri unakwisha, wema hauishi. Sasa jana sikumuona Mheshimiwa Cecil Mwambe hapa mume leo wote hawapo, sasa inawezekana wanafuatilia cheti cha ndoa. *(Kicheko)*

Katibu!

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, jiandae Mheshimiwa Mafuwe, jiandae Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru sana kwa kupata nafasi ya kwanza katika

uchangiaji wa leo. Kwanza kabisa napenda nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kupata tuzo ambayo imeiheshimisha nchi yetu kimataifa. *(Makofi)*

Pili, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mama yetu Mabula, Naibu wake Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Katibu Mkuu na iongozi wote wa Wizara, kwa kweli kazi kubwa wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mchango wangu nianzie katika suala la *muster plan,* sasa hivi nchi inajitahidi sana na hasa Wizara kuhakikisha kwamba *master plan* zinakaa vyema katika nchi yetu, lakini mimi ningependa tu niwashauri Wizara hii *master plan* wasiziachie Halmashauri zetu, waibebe moja kwa moja Wizara ndio washughulike nayo, kwa sababu Halmashauri zetu fedha zenyewe ni za kuokoteza na zina mambo mengi kwa hiyo miradi ya *master plan* katika Halmashauri tukiiachia miradi hii itachelewa sana kufanyika kwa sababu uwezo wetu ni mdogo wa kukusanya fedha katika Halmashauri ili tuweze kumudu gharama za *master plan*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Wizara inatakiwa kwamba itoe fedha zote kuhakikisha kwamba *master plan* zinakuwa katika miliki yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nilikuwa nataka kuzungumzia ni suala la Serikali kuchukua ardhi za watu bila fidia. Imekuwa ni tatizo sugu sasa Serikali kuchukua ardhi pasipo kulipa fidia, mfano mmoja ni kule kwangu Bagamoyo *EPZA* wamechukua ardhi wa wananchi wa Zinga kwa miaka sasa 13 watu bado hawajalipwa fidia, lakini *EPZA* ipo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, lakini katika hili dhambi zote na lawama zote zinawaangukia Wizara ya Ardhi kama vile wao ndio wahusika wakuu, lakini wao kazi yao ni kupima tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niwaomba Wizara ya Ardhi mjaribu sasa hivi kuangalia kwamba mtakapowapimia...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge wa Bagamoyo kwamba mchango wake mzuri sio tu eneo la Bagamoyo, *EPZA* kwenye kanda zote kumi ambazo wamechukua wameendeleza Kanda tatu tu, na hawajalipa maeneo mengi zaidi ya miaka kumi ikiwepo na Kata ya Guta, Bunda Mjini, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Muharami taarifa?

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa, kwakweli hali inahuzunisha na inasikitisha ukienda kwa wakazi wangu wa Mlingotini wakazi wa Zinga, wakazi wa Pande, wakazi wa Kondo, wana malalamiko makubwa sana kuhusu *EPZA* miaka 13 sasa bado hawajalipwa na unakuta unakwenda kuongea na wazee mtu unamkuta mzee ana umri wa miaka 70 analia anatoa machozi, haki yake hajapewa bado eneo limezuiwa hawezi kuuza, akienda ardhi anaambiwa eneo hili limeshawekwa *GN* ni mali ya Serikali hauwezi kufanya chochote. Sasa hii kwa kweli mimi naomba sana Serikali iliangalie upya Wizara ya Ardhi msiwapimie *EPZA* wala *TIC,* wahakikishe kwamba fedha ipo ubaoni ya kulipa wananchi ndio muwapimie, vinginevyo mtabeba lawala ninyi wakati nyinyi mnafanya kazi yetu kwa uzuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la migogoro ya ardhi; migogoro ya ardhi bado ni mingi kiasi kwamba inaanza kupungua Wizara inajitahidi sana, nimpongeze sana Waziri aliyepita Mheshimiwa Lukuvi kazi

kubwa aliifanya alikuja kwangu tarehe 19 Julai, 2021 kwa kweli tulifanya mikutano kama miwili mikubwa sana na wananchi na aliwatia msukosuko baadhi ya watu kiasi kwamba kidogo mambo sasa hivi yanaanza kutulia, kwa kweli wanajitahidi sana Wizara katika kuhakikisha kutatua migogoro ya ardhi bado ni mingi, halafu wajitahidi kuzielekeza na kuzishawishi Mahakama za Ardhi kuhakikisha kwamba wanafanya kazi zake kwa uharaka zaidi maana yake masuala ya ardhi yanapokuwa mahakamani yanachukua muda mrefu, yanachukua miaka mingi kiasi kwamba haki za watu zinakuwa zinapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ninataka kuzungumzia suala la wananchi wangu la Lazaba Makurunge, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri umekwenda kule, umezungumza na watu wa Batini, lakini Lazaba inatatizo kubwa, wananchi wengi la Lazaba walikuwa wakiishi katika ardhi ya Serikali ambayo mwaka 2016 Mheshimiwa Rais Hayati Magufuli alimkabidhi mwekezaji *Bagamoyo Sugar* ambaye ni Bakharesa hekta 10,000 ambazo zilikuwa zikiishi watu ndani yake. Baada ya kukabidhi fidia zikafanyika, lakini wananchi wale hadi sasa bado wana tangatanga hawana pa kukaa, wanakaa katika eneo la Serikali bado na hadi sasa hawajielewi wanakwenda wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lile la Lazaba lilikuwa na hekta 28,000 hekta 10,000 amepewa mwekezaji, hekta 6,000 ni mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hekta 12,000 bado zimebaki mali ya Serikali. Kwa hiyo niiombe Wizara iwafikirie wale watu japo kuwapa hekta 1,000 tu waweke makazi kwa sababu hadi sasa yule mwekezaji bado anapata changamoto ya kupata rasilimaliwatu, anaenda kufuata rasilimaliwatu kilometa 25 wakati pale wangepewa makazi watu ambao jirani na mwekezaji watu wangeweza kuishi na wakafanya kazi katika kiwanda ambacho kinajengwa na mashamba ya miwa wakapata riziki zao.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge niombe utulivu, Waheshimiwa Wabunge, tunaomba utulivu ndani ya Bunge,

wanaosimama na kutoka watoke kwa stahiki na staha za Kibunge, Mheshimiwa muda wako umekwisha. *(Makofi)*

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe, jiandae Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara ya Ardhi, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa tuzo alizozipata, lakini pia kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya CCM anayoendelea nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nimpongeze Waziri wetu kwa kazi kubwa anayofanya kwenye wizara hii lakini nimpongeze Naibu Waziri shemeji yangu kwa namna ambavyo wanasaidiana na qaziri kusogeza gurudumu hili kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitazungumza polepole sana kwa sababu nina jambo kubwa ambalo ningetamani Mheshimiwa Waziri lifikie mwisho sasa, jambo hili ni mgogoro wa *KIA*. Mgogoro huu upo kati ya uwanja wa *KIA* na wananchi waliopo kwenye eneo lile na kihistoria sote tunafahamu uwanja ule ni miongoni mwa uwanja mkubwa wenye eneo kubwa kuliko viwanja vingine Tanzania. Uwanja wa kwanza ni *KIA* ambao una hekta 11,085 ukifuatiwa na Dodoma, Songwe halafu wa Dar es Salaam ni wanne lakini uwanja huu ulipatiwa hati yake tarehe 20 Aprili, 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati uwanja huu unapata hati hizo kijiji cha *Sanya Station* ambacho kina hekta 221.3 kilikuwa kimeshasajiliwa tarehe 18 Agosti, 1976 kwa barua yenye Kumb. Na. KM/VC.295 wakati huo huo kijiji cha Tindigani kilikuwa kimesajiliwa tarehe 1 Februari, 1999 kwa barua yenye Kumb. Na. KM/KGI/477 na eneo lake lilikuwa ni hekta 12,000.37.8. Kijiji cha Mtakuja kilikuwa kimesajiliwa tarehe 18 Agosti, 1976 kwa barua ya Kumb. Na. KM/KG/285 na ukubwa

wake ulikuwa ni hekta 3,859.8. Kijiji cha mwisho ni Chemka kijiji hiki kilisajiliwa tarehe 1 Februari, 1999 kwa barua Kumb. Na. KM/KG/504 ukubwa wa eneo hili ni hekta 778.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kilichotokea ukitazama ni kweli kabisa sisi wananchi wa Jimbo la Hai tunapenda sana uwanja wa ndege wa *KIA* na tunauhitaji sana hatuna shida kwenye hilo, lakini tunafahamu kwamba vijiji hivi vilikuwepo mgogoro huu umetengenezwa na Serikali yenyewe ndiyo waliotoa hati kwenye vijiji na ndiyo waliotoa hati kwenye uwanja wa ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe sana kwa dhati wananchi wale waliopo pale *KIA* wanapata taabu, wanaishi kwa mashaka mashaka juzi hapa mliona walienda kuwekewa alama ya "X" bila kushirikisha hata viongozi, nikauliza swali humu nikapewa majibu kwanini wamefanya hivi, tukasema jambo hili lisijirudie tena, lakini nimeambiwa hapa Mawaziri nane walitembelea Mkoa wa Kilimanjaro bahati nzuri baad ya kuzua taharuki kubwa wananchi wananipigia simu Mbunge tunakuja kuondolewa vijiji vyetu vinafutwa, nikakuona Mheshimiwa Waziri ukanisaidia kutoa ufafanuzi kwamba hapana, hatujafikia hapo jambo hili lipo chini ya Mkuu wa Mkoa.

Sasa mimi niwaombe kwa namna ambavyo nimefanya vikao na uongozi wetu wa Mkoa, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa anayodhamira ya dhati ya kumaliza tatizo hili, tafadhalini sana sisi tunaenda kurudi chini ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kukaa na wananchi kwa kushirikisha viongozi waliopo kule niwepo mimi Mbunge, Diwani, Wenyeviti wetu wa Vijiji na Vitongoji lakini Malaigonan wenzangu (viongozi wa kimila wa Kimasai) ambao ndiyo wengi kwenye eneo lile tushirikiane tuweze kumaliza jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikuombe utakapohitimisha hoja yako uje na kauli thabiti kwenye jambo hili kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, mshauriane ili utoe sentensi wananchi wale wapumue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri jambo hili linanitesa kwelikweli nanila muda mrefu. Wananchi wa Hai narudia tena wanajua umuhimu wa uwanja wa ndege hilo halina shida wapo tayari kukaa mezani tuzungumze tukubaliane hii ya leo tunaahirisha kila siku mgogoro unazidi kukua na watu wanazidi kuongezeka kwenye eneo lile. Mimi niombe ifike mwisho utakapokuja kuhitimisha hapa njoo na majibu jambo hili tunalihitimishaje ndani ya mwaka wa fedha unaokuja tumalize jambo hili na mama yangu kama unanipenda hili jambo ndiyo litakalonisaidia tuendelee kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kwa kazi kubwa waliyoifanya watu wa Hai miaka 15 wakaachana na yale mambo, wakakubali Serikali ya Chama cha Mapinduzi ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati anaomba kura moja ya jambo kubwa alilosema ni mgogoro huu, mgogoro huu usipokamilika pale mnatuingiza kwenye matatizo Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mgogoro huo mkubwa kuna migogoro mingine midogo midogo ambayo mimi naamini Mheshimiwa Waziri hii unaimudu; kuna mgogoro wa shamba namba 240 na 242 Lafofo pale, hili unaliweza ukitenga siku mbili au tatu ukaja ndani ya Jimbo la Hai hii migogoro yote unayoitaja hapo utaimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mgogoro mwingine wa wananchi ambao walitoa eneo lao kwa ajili ya kuruhusu Halmashauri ya Wilaya Hai ijengwe pale, bado wanadai eneo lao, wamezungushwa muda mrefu, wameandika barua muda mrefu, mwisho wa siku ikakubalika kwamba wizara ndiyo isaidie kulipa kwasababu Halmashauri ya Hai haiwezi kulipa fidia ile.

Mimi niombe na hili Mheshimiwa Waziri ulibebe wapo wananchi 19 wakiongozwa na Mzee Philemon Mushi wanahangaika kutwa na matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mgogoro mwingine pia mdogo malalamiko ya wananchi ambao walikuwa wanafanya kazi pale *Lambo Estate,* wengine walipewa maeneo wengine hawakupewa, Mheshimiwa Lukuvi mzee

wangu na *mentor* wangu alianza vizuri sana kazi hii niombe ukamilizie mgogoro huu uishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo mgogoro mwingine huu mgogoro ni kati ya Kijiji cha Uduru na Kijiji cha Mshara na hili tunashindwa kulifanya kule kwetu, ni bahati mbaya sana mwenzangu aliyenitangulia alitoka Kijiji cha Mshara mimi natoka Kijiji cha Uduru, nikienda kuzungumza kuhusu mgogoro huu kunaonekana kuna mgongano wa maslahi. Mimi naomba nikubalie *level* ya wizara ishuke itusaidie kumaliza hapa, kuna wananchi wengi wameweka majumba yao wamekeza miradi yao hawapati hati kwa sababu ya mgogoro huu na ni mgogoro mimi naamini ukishuka wewe mwenyewe pale unahitaji masaa mawili kumaliza huu mgogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme la mwisho katika kuhitimisha tuna mashamba 17 ya ushirika; tumeshazungumza na Waziri wa Kilimo vizuri, niombe atakapokuja mezani kwako tutakapoanza ku-*review* upya mikataba ile na wewe utoe baraka zako na mwisho maombi ya Chemka...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Shekilindi, jiandae Mheshimiwa Kanyasu, jiandae Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja ambayo ipo mezani kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nilitaka kusimama na kutoa mwongozo kwa jambo linaloendelea kutokea kule jimboni kwangu, *panya road* wameingia kule na taarifa nilizozipata juzi na jana naambiwa wameshaua watu watano. Kwa hiyo, naomba Serikali itoe maelekezo juu

ya suala hili ili liweze kukomeshwa mara moja, wananchi wangu waendelee kuishi kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwanza kabisa nimpongeze Rais wetu Mama yetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya na hizi tuzo alizopata. *(Makofi)*

Ndugu zangu nataka niwaambie mtu mmoja aliendа kwa Mtume akamwambia Mtume hivi ninani wa kufanyia hisani au wakumtanguliza kumfanyia hisani basi Mtume akamwambia mama; kisha baada ya mama Mtume akarudia tena akasema mama, ehee baada ya mama akarudia tena Mtume akasema mama. Kwa hiyo, mama ametajwa mara tatu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Baba?

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baba ametajwa mara moja. Kwa hiyo, ona ukubwa wa Mungu ona akina mama walivyopewa uwezo mkubwa mpaka Mwenyezi Mungu anajua mpaka Mitume inajua kwamba mama ndiyo kila kitu kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini soma hata *Surat Mariam* utakuta mama bora ametajwa kwamba ni Mama Mariam ndiyo mama bora na mwanamke bora. Kwa hiyo, ndugu zangu hii tuzo aliyopata mama usije ukasema ni ya kwanza hii ndiyo imeanza zitakuja nyingi na nyingi zaidi kwasababu hii ipo kwenye mikono ya Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nimpongeze mama yangu Waziri wa Ardhi, Mama yangu Mabula kwa kazi kubwa anayoifanya, nimpongeze Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja na watalaamu wote, kwa kweli wanafanyakazi kubwa, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Mama mimi sina mashaka nae kwa sababu ninyi wenyewe mmeyaona kwamba wakati wa Mheshimiwa

Lukuvi ulikuwa unafanya kazi kubwa sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lukuvi amemrithisha mama na tunamuona mama anaenda *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye mchango wangu sasa. Kwanza nianze kuishukuru Serikali imetupa shilingi milioni 208 Halmashauri ya Lushoto kwa ajili ya kupima viwanja na kazi ile inaendelea vizuri, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, lakini pia fedha hizi ninazoomba naomba mtoe maelekezo kwa sababu yanayofanyika kule ni tofauti, kule wale wanaoenda kupimiwa hawana elimu yoyote, sasa unakuta wale ambao wanapima wanapita juu juu tu, mara siku moja, siku mbili tayari ina maana lile lengo halitimii. Kwa hiyo, niombe maelekezo yatoke kwa ajili ya watu wale wapewe elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapo hapo nichangie mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, tumezunguka karibia nchi nzima hii tumeona changamoto, changamoto kubwa iliyokuwepo ni kwamba sheria hizi zinakinzana na nimeona kwenye taarifa ya Waziri kwamba Sera ya Ardhi inakuja. Sasa niombe sheria hii iharakishwe haraka sana ili kuweza kunusuru kwa sababu sasa hivi tukisema kwamba tunamlaumu maana kila lawama inakwenda kwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, TAMISEMI inasheria zake, Madini inasheria zake, Kilimo inasheria zake, Mifugo inasheria zake, Maji inasheria zake, na Maliasili inasheria zake, lakini lawama ikitokea inatupiwa kwenye Wizara ya Ardhi. Mimi niombe sera hii ije haraka sana Sera ya Ardhi sheria hii ije haraka sana iletwe Bungeni ili tuweze kuipitisha ili tumpunguzie uzito, mzigo mama yetu Mama Angelina Mabula, Waziri wetu wa Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili kuna hizi Halmashauri kukopeshwa fedha, zinakopeshwa fedha mwisho wa siku hazirejeshi zile fedha kwa wakati, baada ya kupima viwanja na kuuza viwanja Halmashauri badala ya

kurejesha fedha Wizarani basi wanabaki nazo na wanatumia kwa matumizi mengine, hii siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali sasa kwamba ikiwezekana kuwe na mkakati maalumu wa kurejesha fedha hizi kwa wakati ili fedha hizi zikirejeshwa na wengine waweze kupata na hii itakuwa salama sasa kwa kuharakisha kupima vijiji vyetu kwa uharaka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hii asilimia 30 ambayo ipo kisheria kwamba mtu anapopewa mradi Halmashauri husika basi asilimia 30 iende Serikali kuu mimi niishauri Serikali kwamba asilimia 30 hizi zirudi kule kule pamoja kwamba zipo kisheria lakini sheria ile iletwe tui-*review,* tuifanyie *amendment* ili fedha hizi ziweze kurudi kule kule Halmashauri. Sasa hivi tunalalamika kwamba vijiji vyetu havipimwi, tunalalamika kwamba ina maana upimaji umekuwa ni mdogo sana, lakini fedha hizi zikirudi tayari zitaenda kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine Mheshimiwa...

*(Hapa kengele ililia kushiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Shekilindi mtaalamu wa dawa za *Covid*.

Mheshimiwa Kanyasu, Mheshimiwa Kamonga, Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi, jana sikupata nafasi ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa tuzo aliyopata kama mwanamke wa kwanza na ambayo imetuheshimisha sana sisi Watanzania, lakini pia imeendelea kuifanya Tanzania kuonekana kwamba kidiplomasia tunaendelea kunawiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais alisema yeye hastahili tuzo ile, mimi naomba kusema kwamba kama tungepata Rais asikubali kuendeleza yale ambayo alikuwa anaendeleza Rais mtangulizi, maana yake angeanzisha ya kwa kwake mengine leo tungekuwa na migogoro kwenye miradi mingine iliyokuwa inaendelea. Kwa hiyo, mimi nampongeza sana kwa kuyaendeleza yote na kwa juhudi kubwa na kwamba tuzo hiyo inamstahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siku mbili zilizopita nilisema kwamba Geita Mjini tulikamilisha uandaaji wa *master plan* na *master plan* ya Geita Mjini tuliikamilisha mwaka 2020 na ilitugharimu zaidi ya shilingi milioni 400. Sasa nimuombe Mheshimiwa Waziri kuwa na *master plan* ni jambo linguine, ninaona bado maoteo ya makazi yaholela yanaendelea kuwepo katika maeneo ya mengi ya mji pamoja na uwepo wa *master plan* kwa sababu maeneo mengi ya miji pamoja na kuwa na *master plan* yanachelewa sana kupimwa na matokeo yake yasipopimwa watu wanajijengea vyovyote vile na baadaye tunashindwa kupitisha miundombinu.

Kwa hiyo, juhudi zilizoanza za kutoa fedha katika baadhi ya Halmashauri na tunaipongeza Serikali kwa juhudi hizo tunaomba atukumbuke na atupatie pia Geita Mjini tuweze kupima maeneo yote ili kuweza kuepuka mji ule kuja kujengwa holela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeomba kuchangia kwa jambo moja mahsusi tunazo sheria mbili, Sheria ya Madini inatoa *surface right* kwa mtu mwenye leseni ya kuchimba na anapopewa *surface right* anatakiwa kwa mujibu wa Sheria za Ardhi aidha, awafidie wananchi walioko pale au amalizane nao ili kuweza kumiliki eneo lile.

Sasa tumekuwa na mgongano wa Sheria ya Madini na Sheria ya Ardhi kwenye Mji wa Geita, tunayo mitaa saba; Mtaa wa Katoma, Mtaa wa Compound, Mtaa wa Nyamalembo, Mtaa wa Samina, Mtaa wa Nyakabale na Mitaa ya Katumaini ambayo kwa miaka 23 imeshindikana

kuwapimia wale wananchi waweze kupata hati, tuweze kupitisha miundombinu kwa sababu wanapokwenda kuangalia kwenye kumbukumbu wanakuta kwamba eneo lile linamilikiwa na mgodi, lakini kimsingi mgodi unamiliki *surface right*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, alikuja Mheshimiwa Waziri akiwa na Kamati ya Mawaziri wa Nane, Mheshimiwa Lukuvi, akatoa agizo kwa Kamishna wa Ardhi wa Mkoa ambaye anafanya kazi yake vizuri sana, Mheshimiwa Waziri naomba nikuhakikishie Kamishna anatoa ushirikiano mzuri sana, anafanya kazi yake vizuri sana na ametusaidia sana kumaliza migogoro kwenye eneo letu lile pale. Lakini tumeshindwa kuendelea mbele kwa sababu inaonekana kisheria eneo lile ambalo tayari lilikwishatolewa haki ya kumilikiwa na watu wa mgodi haliwezi kumilikishwa tena kwenye mamlaka zingine kwa watu wengine kwa wamiliki wengine wananchi wa Jimbo la Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokumilikishwa kwa wananchi kwa eneo hili kunasababisha adha nyingi chache zifuatazo; tunazungumzia maeneo ambayo yako kwenye kata tatu ambayo yanahitaji shule, lakini huwezi kwenda kujenga shule kwenye eneo ambalo huwezi kulipima, tunazungumzia maeneo ambayo wananchi wapo wamekutwa na mgodi, lakini ni katikati ya mji hatuwezi kupima kuwapa hati waweze kutumia hati kujiendeleza na kupata mikopo kwa sababu kila unapotaka kwenda kupima watu wa ardhi wanasema mchoro unagongana na mchoro mwingine kwa hiyo, haiwezekani kupima. Lakini siyo hivyo tu maisha ya wananchi katika mitaa hiyo kila siku polisi wanapita, kila siku mgambo wanapita, kwa hiyo, ukichimba choo unaonekana unachimba madini, ukiwa na mifugo umeingia kwenye eneo la mgodi, ukilima unaonekana umeingia kwenye eneo la mgodi. Wananchi wameishi kwa mateso makubwa kwa takribani tangu mwaka 1999. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kwamba sheria zetu zinauwezo wa kulimaliza jambo hili haiwezekani jambo moja Rais wa sasa akiwa Makamu wa Rais alikuja akalitolea

maagizo, akaja Hayati Rais Magufuli akalitolea maagizo, Mawaziri wote waliopita kwenye Wizara hii wanakuja kutoa maagizo lakini jambo haliishi. Nafahamu juhudi za Mkuu wa Mkoa ameitisha kamati mbalimbali, amekutanisha watu wa TAMISEMI, wamekuja watu wa madini, wamekuja watu wa Wizara yako lakini bado hatufiki mwisho. Ni jambo gani hili halifiki mwisho!

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyofahamu mimi haki ya wananchi wale kumiliki ardhi ni haki yao ya kiasili, walikutwa pale na mgodi, mgodi ukapewa leseni, hatuna tatizo na mgodi tunaupenda, kama wanapenda kumiliki lile eneo basi tuko tayari lile eneo wawalipe fidia wananchi waweze kulichukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama lile eneo bado hawajafikiria kuliendeleza watuache tulitumie tunavyotaka mwisho wa siku wakilihitaji waje watulipe. Haiwezekani kwa miaka 20 umeweka matangazo hamruhusiwi kujenga eti leo katika nchi yangu ardhi, ya kwangu nikitaka kujenga lazima nikaombe kibali mgodini ndiyo sheria inavyosema.

Mheshimiwa Waziri nimesimama kuchangia jambo hili, ninaamini ofisi yako ina uwezo wa kulimaliza kisheria, kwa kutumia sheria zilizopo na kama hazipo tuangalie upya sheria zetu ili tuweze kumaliza jambo hili, ni kikwazo kikubwa sana kwa maendeleo ya wananchi wa mitaa saba ya Mji wa Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la mwisho, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Serikali imeridhia kuwaachia zaidi ya vijiji na vitongoji 900. Sasa kinachonisikitisha kidogo, Kata yangu ya Mgusu, Mitaa ya Nyakabale pamoja na Manga...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu ahsante kwa mchango mzuri sana, kengele ya pili.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**NaIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga, jiandae Mheshimiwa Hawa Mwaifuga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Ardhi. Nami niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kupewa tuzo, maana yake mchango wake umetambulika duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Mama yangu Mheshimiwa Angeline Mabula na Naibu wake Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na niwaambie kwamba wananchi wa Ludewa wanawashukuru sana kwa kuwapa fedha kwa ajili ya kurasimisha makazi kiasi cha shilingi milioni 400 na zaidi ambazo zimetumika pale Mlangali wameshapima zaidi ya viwanja 3,000. Halikadhalika Makao Makuu ya Wilaya Ludewa kazi ya upimaji inaendelea. Kijiji cha Amani wananchi wanawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa baadhi ya maeneo wanamashaka na kwamba tunavyopeleka mipango miji watu wa *TANESCO* wanadhani wanataka kuwaongezea bei ya umeme yaani maeneo yale ambayo yamepangwa kuwa *planning areas* watu wa *TANESCO* wana-*charge* gharama kubwa za umeme. Lakini tunaendelea kuwaelimisha na wanawaalika sana kwenda kuwatembelea na wanawaomba mshirikiane na Waziri wa TAMISEMI kuhakikisha watu wa *TARURA* wanasaidia kufungua zile barabara ili Mji wa Mlangali uweze kuwa wa kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Amani ambao wanasubiri sana uwekezaji mkubwa wa Liganga napo paweze kuwa na mji wa kisasa kwamba tusiishie tu kurasimisha, wanaomba tuwasaidie kuhakikisha kwamba barabara zinafunguliwa vizuri ili miji iweze kuwa na mvuto wa

kisasa na vilevile wanaomba sana taasisi mbalimbali za kifedha ambazo zinawezesha wananchi kwenda kutoa mikopo kama *TADB* na *CRDB* waweze kwenda kuwakopesha pembejeo za kilimo. Kwa sababu sasa Wizara ya Ardhi imeongeza thamani ya ardhi yao kuhakikisha kwamba wanapata hati. Kwa hiyo, hongera sana Mheshimiwa Waziri, wananchi umewatengenezea furaha pale Ludewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika Mheshimiwa Waziri wananchi wa Ludewa wanaomba sana pale Makao Makuu ya Wilaya kulikuwa na eneo la kituo cha mabasi na kulikuwa na soko, kulikuwa na vibanda vimegawanywa kwa wananchi waweze kujenga na kufanyia biashara, ni kama uwezeshaji wa kuchumi kwa wananchi. Sasa bahati mbaya kumetokea hali ya kutoelewana kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa na wananchi wale wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wanaomba sana umtume Kamishna wako wa Ardhi aweze kwenda pale na ikiwezekana utolewe muongozo ambao utaonesha haki na wajibu wa kila upande katika kumiliki viwanja hivi vya maeneo ya *stand* na soko, vibanda vya biashara, kwamba ukitolewa mwongozo utaepusha migogoro, wananchi kupelekana mahakamani na Serikali kwa sababu wananchi ni mali ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze pia kwa bajeti hii nimeweza kuipitia vizuri. Nimeona mikakati ya Wizara ya Ardhi ni mizuri sana, mipango yao imekaa vizuri ila sasa uwezeshwaji, Serikali inapaswa kuunga mkono sana Wizara hii tuweze kuwaongezea bajeti kwa ajili ya kuweza kupima nchi hii. Kwa uzoefu nilionao, mimi naamini kama Wizara ya Ardhi itawezeshwa kwa fedha na vifaa kuweza kupima nchi hii kama mipango yao ilivyo, tutapunguza migogoro ya ardhi kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kama ardhi inakuwa imepimwa, mwananchi amelindwa kwa kupewa hati miliki, ni nani atakuja pale kwenda kuvamia eneo la

mwananchi? Kwa sababu itakuwa hata rahisi kutatua migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba sana Serikali iweze kuwaongezea fedha Wizara hii ili waweze kufikia malengo ya kupanga, kupima nchi hii ili kuweza kuepusha migogoro, lakini vilevile kuwawezesha wananchi kiuchumi. Wananchi wanakuwa na dhamana ambayo inawatambua, inawafanya watambulike kwenye taasisi mbalimbali za fedha nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nimepitia hotuba ya bajeti hii ukurasa wa 174, nimebaini Wizara hii ina upungufu mkubwa sana wa watumishi. Naomba nitoe mfano hapa, kwa upande wa Maafisa Ardhi mahitaji ni Maafisa 1,206 waliopo ni 605, upungufu ni watumishi 601, kwa hiyo, waliopo ni asilimia 50.2 ya mahitaji. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iweze kutoa vibali vya ajira ili maafisa hawa, kwa sababu mitaani wamo. Chuo cha Ardhi - Tabora kinazalisha wale Maafisa Ardhi Wasaidizi wazuri, Chuo cha Ardhi Morogoro na Chuo cha Ardhi Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba vibali viweze kutolewa kwa sababu hata hawa Wapima ambao tunatarajia hizi fedha tunazopeleka wao ndio watakaoenda kufanya kazi. Mahitaji ni Wapima 1,978; Wapima waliopo ni 618, upungufu ni 1,360. Kwa hiyo, naomba Serikali iweze kuangalia jambo hili kama tatizo ili iweze kuajiri wataalam. Hata halikadhalika wa Mipango Miji naona nao mahitaji ni 1,036, waliopo ni 330, upungufu ni 706, waliopo ni asilimia 22 ya mahitaji yote. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iweze kutoa vibali ili tumuongezee nguvu Mheshimiwa Waziri na Naibu wake Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete waweze kutimiza malengo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika kule Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi; nashukuru naona na Ludewa wameikumbuka tunaweza kupata hapo vijiji vichache. Naomba sana nao waweze kuongezewa fedha ili waweze kupanga mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kuepusha muingiliano wa watumiaji mbalimbali wa ardhi. Hii

itasaidia sana kuepusha migogoro ya ardhi na niwapongeze kwa kuanzisha ofisi za Kanda. Naomba wazisimamie vizuri ili ziweze kupanga na kupima vijiji, ile mipango kina ya vijiji iweze kuandaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba sana Wizara hii ya Ardhi iweze kushirikiana na watu wa *TRA,* ile kodi ya majengo uaami ule utaratibu tuliouweka mwaka jana kwamba tuta-*charge* kupitia LUKU, mita zile za umeme. Pale nafikiri hela nyingi bado hazikusanywi, kwa hiyo, naomba tuweze kutumia wataalam wetu kuhakikisha mapato yale tunaweza kuyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kutakuwa na mechi ya kirafiki ya mpira wa pete kati ya Waheshimiwa Wabunge Wanawake na Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania. Mechi hiyo itachezwa siku ya Jumamosi tarehe 28 Mei, 2022 saa 10.00 jioni katika uwanja wa Jamhuri. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa sana kuhudhuria mechi hiyo.

Mheshimiwa Hawa Mwaifuge, jiandae Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naitwa Hawa Mwaifunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na nimeweza kusimama tena katika Bunge hili na mimi niweze kuchangia hoja ya Wizara hii ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Wabunge wenzangu wametangulia kuzungumza nami naomba niseme mambo yafuatavyo; naomba na mimi nijielekeza kwanza

kwenye hii Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume hii kwangu mimi ndiyo niliona muarubaini wa kupunguza migogoro ya ardhi katika nchi hii. Lakini tume hii ina sheria nzuri, tume hii imejiandaa vizuri katika kutekeleza majukumu yake, tume hii ina kiongozi mzuri ambaye ni Profesa na maandiko yao ni mazuri kabisa ukiyaona kwenye makaratasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini changamoto kubwa iliyopo ni ukosefu wa fedha. Haiwezekani nchi hii ikatulia, nchi hii ikapata amani ya migogoro kama tume hii haijaingia kazini kwenda kupanga matumizi ya ardhi kwenye vijiji vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwenye Ilani yenu ya Chama cha Mapinduzi mmesema angalau kila mwaka vijiji 750 viende vikapimwe. Leo mnatoa fedha ya vijiji 100 vikapimwe, hivi vijiji 3,000 ambavyo mnasema ndani ya miaka mitano viwe vimeshapimwa vitafika lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu mnapotoa fedha huwa mnaangalia kwanza Ilani halafu ndiyo mnakwenda kutoa fedha. Sasa kwa nini hii tume imewekwa nyuma wakati imo ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi? *(Makofi)*

Kwa hiyo, niombe sana kama ambavyo wenzangu wamesisitiza, tunaomba sana Kamati ya Bajeti, Serikali, Waziri wa Fedha wakae, waangalie namna bora ya kuweza kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mama Mabula aweze kufanya kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu inafika mahali Wabunge tunashindwa kuzungumza vizuri kwa sababu tutasema nini wakati huyu mama bado hajapewa fedha? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hebu mpeni fedha, halafu ashindwe kufanya kazi ili tusimame hapa tuseme. Kwa sababu sasa hivi hata tukisema tutakuwa tunamuonea na huku ndiyo kwenye eneo mahususi ambalo anaweza kufanya kazi vizuri na kwenda kupunguza migogoro ya ardhi iliyokuwepo. Wanapambana sana kupunguza hii migogoro. Leo kuna Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya, kuna Mabaraza ya Ardhi ya Kata, kama hii tume ikiwezeshwa hata haya mabaraza yatakuwa hayana kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na huku kwenye mabaraza kesi nyingi sana unazokutana nazo za migogoro ya ardhi wengi wanaoteseka ni wakinamama tena wajane. Ifike mahali tuwaonee huruma hawa wanawake, kwanza wamefiwa na wanaume zao, lakini pili bado wanapambana na migogoro hii ya ardhi. Kila siku kwenda na kurudi kwenye haya Mabaraza ya Ardhi kwa kweli ni mtihani mkubwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niombe sana na mimi kama Mjumbe wa Kamati hii na tulishaomba na ninarudia tena, bila fedha hizi kuwapa hawa tume, hakuna kitu kitakachoweza kufanyika kupunguza migogoro hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe shilingi bilioni 10 walizoomba siyo nyingi, ni hela kidogo sana kama alivyozungumza ndugu yangu jana hapa, ni hela kidogo sana ambayo Serikali haishindwi kutoa hii fedha ili hawa Mawaziri na watendaji wao waende wakafanye kazi. Tunahitaji angalau vijiji 750 angalau viweze kupimwa jamani tupunguze hii migogoro kupangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tumekwenda Singida Vijijini, Kijiji cha Ntondo na Kijiji cha Nkwae tumejionea wananchi wale wakiwa na furaha baada ya kupangiwa maeneo yao. Kwa hiyo, sasa hivi hakuna mtu anayeweza kwenda kuvamia pale Nkwae na Ntondo. Kwa sababu wale wananchi wameshatengenezewa mazingira mazuri na kila unayemuuliza anakwambia hapa ni hiki, hapa ni hiki, hapa ni hiki, hapa ni hiki. Nani atakuja kuvamia? Ili tupunguze hata

mauaji ya wakulima na wafugaji? Tupange matumizi bora ya ardhi, hakuna mtu atakayeweza kuja kuvamia kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Mawaziri Nane; mimi nipo kwenye Kamati ya Ardhi na tuliomba hapa na kuna mwenzetu mmoja aliomba mwongozo. Kamati hii ilikuwa haijawahi kutoa taarifa, tulivyoomba walikuja wakatupa taarifa kidogo. Kwa taarifa ile ambayo wametupa, ninachokiona badala ya kwenda kutatua changamoto za migogoro ya ardhi tumekwenda kufukua moto ambao sijui huko mbele hali itakwenda kuwa namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawaziri nane wanapokwenda kwenye Majimbo ya watu na kwenye Mikoa ya watu waonane na wananchi na siyo kuishia kwenye Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, waende kwa wananchi. Wanakwenda kwa wananchi wakikuta sehemu imetulia, lakini wakikuta sehemu moto unafuka, hawaendi wanaishia kwenye Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Inawezekana kabisa hii Kamati ya Mawaziri Nane ikawa ni mwiba mchungu kwa wananchi kuliko ilivyo kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa dada yangu Angeline Mabula mkienda kule, nendeni mkawaone wananchi waambieni ambacho mnakwenda kukifanya. Zile kamati zetu ndogo mnazoziacha kule chini ndiyo mwiba mchungu kwa wananchi na kila siku nawaambia mtakuja kukuta mambo ambayo hamkuyategemea huko chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la kurasimisha. Hili jambo sisi labla pengine kama Wajumbe wa Kamati tunaweza tukawa tumelielewa na baadhi ya Wabunge. Lakini wananchi huko hawalielewi hasa wananchi wa Jiji la Dar es Salaam. Naomba sana watakapokuja ku-*windup* hapa waeleze hili zoezi la kurasimisha lina maana gani na nini kifanyike ili wananchi wale waweze kulielewa, vingingeno mtakuwa mnatangwa maji kwenye kinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naomba. Wizara hii inahitaji wafanyakazi. Waongezewe wafanyakazi ili kazi ziweze kufanyika kwa ufanisi mkubwa kuliko ilivyo hivi sasa, wafanyakazi ni wachache, kazi ni nyingi, wanahitaji kufanya mbambo mengi kuliko uwezo walionao wa wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la mwisho naomba nijikite kwenye Mkoa wangu wa Tabora, hususan kwenye Manispaa ya Tabora Mjini ambako mimi ni Diwani kwenye Manispaa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Tabora Mjini waliamua kutoka mjini na wakaenda kwenye eneo la nje ya mji ambalo linaitwa Ndevelwa. Eneo lile limepimwa viwanja na wananchi wamepewa hati. Lakini watu wa *TARURA* mpaka sasa bado hawajapeleka miundombinu ya barabara ili wananchi wale waweze kuonyeshwa maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Wizara ya Ardhi mshirikiane na Wizara ya TAMISEMI, watu wa *TARURA* wapeleke barabara ili wananchi waweze kuoneshwa maeneo yao. Haiwezekani mtu ana hati mkononi halafu eneo lake halijui, eneo langu ni lipi. Kwa hiyo, naomba sana watu wa Wizara hakikisheni wananchi hawa wanajua ili watu waweze kulipia zile hati, tuweze kupata fedha kwa ajili ya kutatua migogoro iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naliomba, naomba sana na naomba nisisitize sana kwa Wizara, fanyeni ukarabati kwenye nyumba za *National Housing,* yamekuwa kama magofu, tumechoka kuona hali hizi ikiwemo kwenye Manispaa yangu ya Tabora, yaani zile nyumba zimezeeka pamoja na kwamba Tabora ni mji mkongwe lakini tunaomba mtusaidie zile nyumba zenu pale ziko nyingi lakini zote hazifai zimechakaa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Ahsante kwa mchango. Ahsante, unga mkono hoja.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Unga mkono hoja.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbogo, jiandae Kitandula, jiandae Mtemvu.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Ardhi. Kipekee kabisa nimpongezee Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na kipekee zaidi Mheshimiwa Rais kwa kupata tuzo kwa sababu nchi za nje zimetambua mchango mkubwa wa maendeleo anayowaletea Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hizi tatu, TAMISEMI, Maliasili na Ardhi ndiyo chanzo cha migogoro kwa wananchi, kwa sababu hizi Wizara hazikai pamoja zikaja na muelekeo mmoja wa namna ya kutatua migogoro kwa wananchi. Kila Wizara inafanya kazi kivyake, kuanzia sasa hivi wanatakiwa wakae pamoja, waje na jibu moja namna ya kutatua migogoro kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu lina kata 11, kata sita zote sehemu ambayo ni salama haina migogoro ni Makao Makuu ya Kata; Vijiji vyote vinavyozunguka kwenye hizi kata sita vyote vina migogoro ya ardhi. Ukigeuka huku kuna ranchi, ukigeuka huku Hifadhi ya Lwafi, hii Hifadhi ya Lwafi wananchi wa Jimbo la Nkasi Kusini pamoja na Rukwa ni wakulima. Lakini hizi hifadhi wananchi wameongezeka, lakini sehemu ya kulima wanapata tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Ridhiwan - Naibu Waziri, baada ya kikao cha Bunge *break* ya kwanza njoo Rukwa kuna migogoro mikubwa sana ya ardhi, umasikini wa Mkoa wa Rukwa unachangiwa na migogoro ya ardhi. Njoo utataue migogoro ya ardhi Mkoa wa Rukwa ili wananchi waweze kufanya kazi, waweze kulima kwa amani kwa sababu ni wachapakazi ili wanakwamishwa na migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano Jimbo langu la Nkasi Kusini, vijiji vya Mkukwe, Kwamachindo, Mkata, China, King'ombe, Nundwe, Yasimba, Tundu, Tolesha, Izinga, Mwinza, Yela, Kwemanchindo hawa wote wako ndani ya hifadhi, akigeuka huku ni Ranchi ya Mkalambo, akigeuka huku Ranchi ya Nkundi; kwa mfano Ranchi ya Nkundi ni shamba la mwekezaji. Kijiji cha Nkundi hakuna hata eneo la kuweza kujenga shule, ofisi, mambo ya kijamii eneo hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri njoo utupatie Kijiji cha Nkundi eneo la kujenga shule kwa sababu hili shamba la Nkundi linapakana na kijiji. Wanakijiji wanahitaji maeneo ya shule, ofisi na mambo mengine ya kijamii pamoja na zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vinavyozunguka mfano Kalambo, *Kalambo Ranch;* Kijiji cha Sintali Komanchindo hawana eneo la kulima linapakana na hifadhi ya Lwasi, mwiba mkubwa zaidi Mkoa wa Rukwa ni shamba la Efatha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Deus Sangu ameongea jana, hii ni ajenda ya Wabunge wote wa Mkoa wa Rukwa huyu mwekezaji amekuja sio kuwekeza, ni udalali, mashamba yanakodishwa, wananchi hawana maeneo la kulima, wakilima anaenda kupitisha trekta heka 100, heka 50 anavuruga mashamba ya wananchi, wananchi wanakamatwa akina mama wakipelekwa mahabusu kesi inaisha mahakamani hawa na lolote wanarudishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Rukwa hasa shamba la Efatha ni mwiba, Kijiji cha Sikaulu wananchi wamekuja kufika hapa sisi Wabunge tumeanza kuhangaika kutatua migogoro ya shamba la Efatha. Mheshimiwa Waziri wewe ni mcha Mungu, Mheshimiwa Ridhiwani tukimaliza hapa njoo anza na Efatha. Unapokuja kuhitimisha uje useme mgogoro wa Efatha unaisha lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa ni wakulima, wanafanya kazi nzuri zaidi, wanahamia shambani kwenda kuweka makambi ili apate muda wa kulima, Wizara inaenda Maliasili wanachomea watu, wanafukuzwa wanaharibiwa mashamba yao hii sio haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara *break* ya kwanza njoo Rukwa uje utatue migogoro ya ardhi Rukwa inachangiwa umaskini kwa sababu Wizara hii haijaitendea haki Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kitandula jiandae Mheshimiwa Mtemvu, jiandae Mheshimiwa Gwajima.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi nichangie kwenye hoja iliyopo mezani. Namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye anaendelea kutupa baraka zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuipongeza Wizara kwa kazi kubwa inayofanya, tulizoea huko nyuma, Wizara hii ilikuwa ni Wizara ya migogoro sana, lakini kadri siku zinavyokwenda tunaona mabadiliko makubwa sana, hongereni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri haya nitakayoyasema sio mageni kwa Wizara, ni mambo wanayoyafahamu naomba wayashughulikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ni tatizo la mpaka kwenye ukanda wa bahari, Mheshimiwa Waziri ulifika Mkinga tukaenda Jasini unajua kilichotokea, tuliingia kwenye nyumba pale, upande mmoja ni Mkinga upande mmoja ni Kenya. Kwa hiyo, changamoto ile unaifahamu. Katika eneo lile hasa kwenye ukanda wa bahari wavuvi wetu wanapata shida kubwa, kila unapoenda kuvua wanaambiwa wameingia kwenye eneo la Kenya, mali zao zinachukuliwa, boti zao zinachukuliwa, wanapelekwa Kenya wanafunguliwa kesi kule. Hiki kimekuwa ni kilio cha muda mrefu cha watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali twendeni tukaweke mipaka twendeni tukaweke maboya yale yaliharibika ili mpaka ule ujulikane kinagaubaga tuondoe tatizo la watu wetu. Pale Jasini askari wa Kenya wanaingia mpaka Tanzania wakikamata watu, hebu tulishughulikie tatizo hili kwa haraka kabla halijaleta madhara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ni tatizo la migogoro ya vijiji na vijiji katika Wilaya ya Mkinga, hili nimelileta kwa maandishi muda mrefu na chanzo cha migogoro ile ya vijiji na vijiji, ni ramani iliyotolewa mwaka 2007 wakati Mkinga inamegwa kutoka Wilaya ya Muheza. Zoezi lile halikuwa shirikishi, wanakutwa kijiji kimoja kijiji cha upande wa pili uongozi haupo, wananchi hawakushirikishwa, kwa hiyo tumezalisha migogoro karibu kila kata, kata na kata kijiji na Kijiji. Naomba hili lichukulieni kwa umuhimu mkubwa twende tukaondoe tatizo lile, kama ni kutafsiri ramani ile twendeni tukatafsiri kwa wananchi wale tuondokane na migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wamefikia sasa wanashikiana mapanga huko, tusisubiri watoane uhai twendeni tukashughulikie tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni eneo ambao tuliomba shamba la Kwantili ambao limetelekezwa kwa zaidi ya miaka 20, shamba ambalo hata ulipaji wa ada ya kodi pale anayemiliki halipi sawasawa, tumeomba shamba hili

lifutiwe hati. Shamba lenye Hati Na. 47 22 lenye ekari 58 na shamba lenye Hati namba 14501 lenye ekari 2,841 tulitoa ilani mwaka jana baada ya kugundua kwamba mwenye shamba huyu aliend a kukopa nje ya nchi na hati zile alizigeuza kuweka dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilani ile imetolewa tangu mwaka jana, imeiva mwaka jana mwezi wa tisa mpaka leo hatujui nini kinaendelea! Mheshimiwa Waziri hili unalifahamu tuliteta kule Tanga Kamishna wa Ardhi alisema anakwenda kuliangalia, hatujapata majibu, tunaomba mtusaidie tufute shamba hili ili ardhi ilejeshwe kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni lile linaloshughulikiwa na timu ya Mawaziri mlipokuja kule Tanga tulieleza, eneo la Kimuni mgogoro ule tulikwisha ushughulikia kwa kina mwaka 2016; Wizara ilituma timu kikosi kazi kikafanya kazi ile tukafanya kazi nzuri ya kushiriki, mikutano ya hadhara na wanavijiji tukafika makubaliano, timu ya uongozi wa mkoa iliyohusisha Mkuu wa Mkoa, Wabunge wa Wilaya zinagusa maeneo haya tulikuja Wizara ya Maliasili tukakubaliana. Tunaomba mnapoenda kufanya maamuzi mapendekezo yale yazingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande wa kule Maramba kuna ahadi ya Waziri Mkuu kwenye shamba la Mwele, Waziri Mkuu alishaahidi wananchi wale watapatiwa ardhi kutokana na changamoto kubwa ya ardhi, tunaomba ahadi ile ya Waziri Mkuu ipewe umuhimu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya nakushukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Mtemvu na mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Gwajima.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kwenye Wizara hii ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kufanya uteuzi mzuri wa dada yangu Dkt. Angeline Mabula kuwa Waziri mwenye dhamana na Wizara hii ya Ardhi na Makazi, lakini pamoja na hilo pia kwa ndugu yangu rafiki yangu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ridhiwani Kikwete kuwa ni msaidizi wa Mheshimiwa Mabula. Lakini nitambue kazi nzuri inayofanya na Wizara, kwa maana ya watendaji wao wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitasema kidogo tu kwenye eneo ambalo mara nyingi nikipata nafasi nalisemea kama kuikumbusha Wizara na eneo lenyewe ni jambo la urasimishaji. Mjumbe mmoja kule upande wa pili alinyanyuka akaweka kibwagizo tu kwamba wananchi wanatakiwa waelewe sana nini maana ya urasimishaji na akatoa mfano yeye anatoka Tabora lakini akasema hasa kule Dar es Salaam, mimi nikapiga makofi hapa mawili matatu nilitaka kumwambia ni kweli tunatamani kujua maana ya urasimishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hiki ni kidonda kisichopona, hili kwetu ni tatizo, mwaka jana nilisema hapa, nilisema tukatofautina tofautiana na Mheshimiwa Waziri akiwa Naibu Waziri, moja kwenye swali la msingi lakini baadaye hata wakati nachangia kwenye fungu hili. Hoja yetu pale tunajua na huku imesemwa kwenye ukurasa wa 43 urasimishaji kwa ujumla katika jukumu la kupanga, kupima na kumilikisha ardhi, sehemu kubwa ni jambo la mamlaka zetu za Miji na Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunatambua kule Dar es Salaam jambo hili wamepewa makampuni kufanya na Mamlaka za Miji haya makampuni tunaanzia hapa, yameletwa na kupewa ithibati kwa kuwa *scanned* na Wizara yaani wananchi wetu kule so tu wamepokea makampuni au walikaa wenyewe wakasema aje huyu au aje yule, Wizara mliangalia makampuni yale, lakini mwisho wa siku mkasema sasa nendeni mkaingie katika Halmashauri zenu za Miji na

Halmashauri na Halmashauri za *I mean* katika miji yetu ili wafanyekazi na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa tatizo, mwaka jana nilisema wizi mkubwa, makampuni yametuibia, fedha nyingi tukatofautiana hapa, lakini mimi nakumbuka Naibu Waziri amekuja juzi tu, kabla ya kuwa waziri wakati mdogo tu kabla hajawa Waziri ameona, kwamba kama tumetofautiana *figure,* lakini zaidi ya bilioni nane aliziona kabisa kwamba iko shida sehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukweli nitumie nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Kheri Dennis James, Mkuu wa Wilaya ya Ubungo nampongeza kwa sababu amechukuwa hatua za awali lakini amepata ushauri baada ya kutembelewa na Mheshimiwa Waziri kwamba tufike sehemu, yale makampuni baadhi yake wakasimamishwa, lakini bado hoja yangu fedha za wananchi ziko wapi, mwaka jana nikasema jicho la tatu lije, hata kama *CAG* nikawashauri mleteni ili ajue hela za wananchi ni kwa kiasi gani zimeibiwa hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwaka jana tuliambiwa mradi huu wa miaka kumi unaenda kuisha mwezi Oktoba 2023; mwaka 2023 ni kesho kutwa sisi bado hela tumepoteza mabilioni ya hela, lakini dhima inasemwa humu, lakini dhima ya kupima, kupanga na kutoa hati, ni kuboresha maisha na uchumi wa wananchi sasa sisi tunafanya nini tunaendelea kuwa maskini hati hatuna, ardhi yenyewe tunakuwanazo kwa shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri kwa haraka; nimeona hapa wewe ni shahidi inazungumzwa miji shilingi bilioni 45.7 huku amesema kama bilioni hamsini hivi zinapelekwa kwenye Halmashauri 25, kwa ajili ya jambo hili hili la kupima kupanga na kumilikisha ardhi, wakati mwaka jana nilisema kila mwaka zinawekwa zinaenda huko, shilingi bilioni 50 wengine wanapewa kwa jambo lile Dar es Salaam inaachwa tena, kwa hiyo wananchi wanatoa wenyewe na wana hali mbaya na zinaibiwa na hatufanyi chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mim niwaombe sana Mheshimiwa Waziri nataka nikushauri na katika hili naomba uniruhusu nimwomba na Waziri Mkuu aliingilie jambo hili na aje Kibamba kwenye Jimbo lile na Wilaya nzima ya Ubungo aone anatutatuaje, pelekeni chukuweni jukumu ile hela yote iliyopota fanyeni ninyi ndio imepotea kwenu kwa sababu mlileta ninyi yale makampuni. Wapelekeeni zile *demand* kwa ajili ya kulipia hati tu, ile ndio wadaiwe wale wananchi ambao wameibiwa zile fedha na yale makampuni mliyoyaleta ninyi huo ndio ushauri katika eneo hilo. Nafikiri nitakuwa nimeeleweka siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili Mlonganzila pale miaka ya nyuma kidogo wananchi watakumbuka tumepeleka pale hospitali ya Mlonganzila kulikuwa wananchi wanaishi katika lile eneo zaidi wa wananchi 2500, eneo lile ambalo kuna Hospitali ya Mlonganzila, lakini mimi nishukuru sana Serikali zetu zote hizi ziliona hiyo sababu ikawalipa mali zao, iwe mazao na nyumba zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa sababu ya eneo hili baada ya tathimini kubwa ilionekana la *Tanganyika Packers* basi wakati ule namkumbuka alikuwa Angellah Kairuki alifika na wakakubaliana kama neno la Serikali kwamba tutawalipa kifuta machozi shilingi milioni mbili kwa kila ekari mwaka 2015/2016 mpaka leo, sijui ni kwa sababu tulikuwa tunaenda kwenye uchaguzi wa 2015 hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri hili jambo mlikumbuke, muende kule wananchi kule wanalia mkalipe kile kifuta machozi mlichokiahidi cha shilingi milioni mbili kwa kila ekari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya mwisho dogo juu ya kuboresha miji ya Dar es Salaam kama maendeleo katika maeneo ya Tandale nilishalisema wakati nachangia Waziri Mkuu, maeneo ya Manzese, maeneo ya Magomeni kama tulivyofanya *Magomeni quarters* tubadilishe uchumi wa Dar es salaam ili maisha ya watu yawe bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gwajima.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hoja hii ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendelea na Makazi.

Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa bidii anazofanya kuzunguka kwenda kila mahali kutupigania sisi Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hoja hii ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi nataka kuzungumzia kwa habari ya migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali Tanzania, lakini kwa kuwa mimi ni Mbunge wa Jimbo la Kawe nataka tu nijikite zaidi kuzungumza kwa habari ya migogoro ya ardhi katika Wilaya ya Kinondoni. Lazima nikiri kwamba Wilaya ya Kinondoni imekuwa ndio kinara wa migogoro ya ardhi inayochochewa na viongozi wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana ku-*note* hilo jambo kwamba inachochewa na viongozi wa Serikali. Viongozi wa Serikali badala ya ku-*solve* matatizo ya wananchi kuna baadhi ya viongozi wasio waaminifu wanachochea migogoro ya wananchi na kuwachonganisha na Serikali yao. Nitoe mfano mmoja; kuna kisa kimojawapo ambacho kimetokea kwenye eneo linaitwa Mbweni Mpiji. Mbweni Mpiji siku moja nikapigiwa simu na Katibu wangu (Katibu wa Mbunge) kwamba kuna matrekta, kuna buludoza zinabomoa nyumba za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikakimbia pale Mbweni Mpiji kwenye Kata ya Mbweni jambo la kusikitisha kweli nilikuta nyumba 103 kubwa zimeanguka chini na mbaya zaidi nikakuta baadhi ya watoto wameachwa kwenye hizo nyumba, polisi wanapiga mabomu, kina mama

wanachapwa viboko na polisi wamejaa kwenye eneo hilo, sikuamini kwamba hii ndio Tanzania ninayoijua, kilichonishangaza ni kutaka kujua nini sasa kimetokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikamuona *OCD* kumuuliza je, kuna oda yoyote ya Mahamaka *(eviction order)* ambayo wewe umekuja kusimamia kubomoa nyumba za wananchi hana, nikawafuata viongozi waliokuwepo pale kama wana hati yoyote hawana, jambo la kushangaza lilikuwa ni hili kwa nini mnabomoa nyumba za wananchi! Wakasema tunabomoa nyumba za wananchi kwa sababu eneo hili kwenye mpango limepangwa kuwa bustani ya miti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbuka haijajengwa hiyo bustani, haipo wananchi wamejenga nyumba zao zaidi ya miaka mitano wanaishi, mtu anakwenda kuangusha chini nyumba za wananchi 103 maskini, wananchi walewale ambao mwaka 2020 tumepita tukiwaomba kura za Mheshimiwa Rais na za Mbunge, leo nyumba zao 103 zimeanguka chini wanawake na wanaume wamekamatwa wamepigwa, huyu polisi/*OCD* anaye-*executive* hii *order* hana *document* yoyote, wanaobomoa hawana *document* yoyote na hakuna hata mmoja mwenye *document. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inashangaza kweli kweli, nikazungumza waliokuwepo Maafisa wa Manispaa, wakasema wameelekezwa na Mkurugenzi wa Halmashauri, nikazungumza na Mkurugenzi wa Halmashauri Dada Hanifa akasema hajawaelekeza, hawana maelekezo yoyote ya kwake, baadaye wakahamia kusema kwamba wamelekezwa na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inashangaza kweli viongozi wa kiserikali waliowekwa kwa ajili ya kutetea wananchi, wanakuwa sehemu ya mgogoro ya kuwagombanisha wananchi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri kukubali kiongozi yeyote ama wa kisiasa ama wa Serikali inayotokana na

Chama cha Mapinduzi jukumu lake la kwanza ni kuhakikisha Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi amekaa kwenye kiti salama na yuko salama katika shughuli zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inapotokea kiongozi ama wa kiserikali ama kisiasa anayetokana na Chama cha Mapinduzi hafanyi jukumu hilo basi huyo ni hujuma juu ya Rais wetu na ni hujuma juu ya chama chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninapoongea sasa hivi Jimbo la Kawe, lina migogoro ya ardhi mingi hakuna anayeonekana kujali kusuluhisha migogoro hii. Nimefurahishwa sana wiki iliiyopita na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi rafiki yangu Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, nilizungumza na yeye pamoja na Mheshimiwa Nape wakaja kwenye Jimbo la Kawe kwenye Mtaa wa Jogoo na Ndumbwi, ambao wananchi walikuwa wamezuiwa kuwekewa *postcode* kwa sababu eneo hilo kwenye mchoro linaonekana eneo la viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbuka ni zaidi 4,500 zimejengwa mle ndani na hakuna kiwanda chochote, hakuna kesi yoyote, hakuna anayewadai, lakini wananchi wamezuiwa kuwekewa *postcode* kwa sababu linasomeka kwenye ramani ni eneo la viwanda, wameishi miaka 30, Mheshimiwa Nape na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete wakakaa pale ndani ya masaa mawili, walishatatua mgogoro ulioshindikana kutatuliwa ndani ya miaka 30 iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwambia Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete pamoja na Mheshimiwa Nape mmefanya kazi nzuri sana na hiyo ndiyo kazi ya kiongozi. *Leadership is making decision wether negative or positive,* ni afadhali kwa kulaumiwa kwa kufanya maamuzi yasiyo sahihi kuliko kutokuamua kabisa kabisa, nawapongeza sana kwa hiyo kazi mliyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi viongozi wengi wa kiserikali wasio waaminifu wanachochea migogoro na kumgombanisha Rais pamoja na wapigakura wake. Kwa mfano, kwa dakika chache tu, kule kuna eneo linaitwa Mwembetogwa Boko Chama jana tu wamefika pale wameleta polisi kuwa-*harass* wananchi, kesi ipo mahakamani lakini wananchi wanakuwa *harassed,* watu zaidi ya 200 wametolewa kwenye makazi na kesi ipo mahakamani.

Ninaomba sana Wizara ya Ardhi mshughulike sana na suala la migogoro ya wananchi ili tumsaidie Mheshimiwa Rais kuwa na kura zake zilizonona katika Jimbo la Kawe na kuondoa uchonganishi kati ya wananchi na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya kwa dharura iliyojitokeza Mheshimiwa Mwita Mwikwabe. Mwita si umeomba kuchangia? Mwita Mwikwabe Waitara ulichangia jana.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilichangia jana, mimi nimeomba kushika shilingi. Jana nimechangia Mheshimiwa au niendelee mambo yapo mengi.

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake kwetu sote, kwani tunajivunia kwa jinsi alivyotuvusha kwenye majanga mbalimbali kwa mfano corona na majanga mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wote wa Jimbo la Mbulu Mjini kutoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,

Rais wetu mpendwa kwa jinsi anavyoiongoza nchi yetu na kusimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM 2020 – 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara na Mheshimiwa Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa jinsi mnavyoitendea haki Wizara hii; kwanza kutusikiliza sisi wawakilishi wa wananchi na kutatua tatizo la kuzuia ujenzi holela na kuleta kupanga, kupima na kumilikisha (KKK) kwa nchi nzima, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naungana na viongozi wenzangu kutoa pole nyingi kwa familia zilizopata msiba ya kuwapoteza wapendwa wao kuanzia kwa viongozi wote, watendaji na Watanzania wote, Mwenyezi Mungu atujalie hali ya ustahimilivu katika kipindi hiki, sote kwa pamoja tunaziombea roho zao kwenye ufalme wa mbinguni usio na mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitoe mchango wangu kupitia hotuba ya bajeti ya mwaka 2022/ 2023 ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali yetu kwa kuleta mpango wa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika Halmashauri zote nchini na kuonesha mafanikio makubwa sana kukabiliana na kuzuia ujenzi holela na kurasimisha ardhi kuwa na thamani kubwa na miji itakayopangika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi kuna baadhi ya changamoto zinazozuia jitihada hizo zikiwemo upungufu mkubwa sana wa vitendea kazi, watumishi wa kada muhimu katika idara za Ardhi ngazi za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba sana Serikali iwaajiri wataalam wa kada muhimu katika kufanikisha mpango huu muhimu sana kwenye bajeti ya mwaka huu.

Tunashukuru sana Serikali kwa kuondoa baadhi ya maamuzi/ hukumu katika Mabaraza ya Kata kwa kuwa baadhi ya walalamikaji na walalamikiwa kutokuridhika na maamuzi ya mabaraza ni muhimu sana Serikali kuwa na mfumo wa kuchunguza mabaraza yanayolalamikiwa hasa kwenye mashauri mengi yanayogusa Serikali za Vijiji, Halmashauri za Wilaya, taasisi za Serikali na watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza sana Serikali kwa mpango wake wa kutumia timu ya Waheshimiwa Mawaziri na watendaji kufanya ziara ya kutatua migogoro nchi nzima. Kwa hiyo ni muhimu sana kabla ya timu hiyo kuondoka wakatoa nafasi kwa waheshimiwa Wabunge wa maeneo hayo kama wawakilisha wa wananchi ili kupata na kuelewa historia na chimbuko lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ijitahidi kukusanya mapato yake ya ndani kwa 100% ili kufanikisha lengo lake kwa mwaka wa bajeti kwani kiwango cha 42% kilichokusanywa mwaka 2021/2022 ni ndogo vinginevyo kufanyike mapitio ya kina kwenye vyanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho siyo kwa umuhimu tunaiomba sana Serikali ijitahidi kutoa fedha zinazoombwa na Wizara hii ili kufanikisha malengo kwani kiwango cha 51% kwa fedha zilizotolewa na Serikali 2022/2023 ni ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa silimia mia moja na naomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Dkt. Angeline Mabula na Naibu Waziri Ndugu Ridhiwani Kikwete pamoja na wataalamu wa Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitachangia kuhusu migogoro ya umiliki ardhi katika Jimbo langu la Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jimbo langu la Moshi Vijijini kuna migogoro ya umiliki wa ardhi baina ya wakulima na wafugaji katika Kata za Mabogini (Kijiji cha Mserekie) na Arusha Chini (Mikocheni na Chemchem) zilizoko maeneo ya tambarare.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro hii imeshasababisha madhara makubwa ikiwemo vifo na uharibifu mkubwa wa mali kama mazao ya wakulima. Mpaka sasa Serikali ya Wilaya na Mkoa haijaweza kupambana na changamoto hii, kwani tatizo hili linajirudia mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya wakulima na wafugaji jimboni kwangu inasababishwa na uhaba unaoendelea kukua wa rasilimali ardhi. Kutokana na hali hii, wakulima wamekuwa wanafungua mashamba kwenye maeneo ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro hii kwa kiasi kikubwa husababishwa na yafuatayo; kwanza Serikali haijayapima maeneo ya wafugaji na wakulima na kuyamilikisha kwa wahusika kwa kutoa hati za kimila na za Serikali.

Pili, kubadilika kwa tabia nchi kunakopelekea malisho kukauka na kusababisha uhaba wa chakula cha mifugo na kuwafanya wafugaji kulisha mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima; na tatu, kupanuka kwa shughuli za kilimo na makazi ya watu ambapo maeneo ya ufugaji yamepungua.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hii ninaishauri Serikali kama ifuatavyo; kutokana na migogoro inayoendelea, kuna umuhimu wa Serikali kuingilia jambo hili na kuhakikisha kuwa maeneo husika yamepimwa na kumilikishwa rasmi kwa wahusika. Pia Serikali iharakishe zoezi hili kwa kutumia mifumo ya hati za kimila zinazotambuliwa kisheria na baadaye wapewe hati za Serikali za kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mazingira ya Kitanzania, ninaishauri Serikali ipitie sera za umiliki wa ardhi

zenye utata zinazoweza kuchochea migogoro ya matumizi ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji. Sera nzuri na rafiki itasaidia kutoa haki bila malalamiko.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali, Wizara za sekta husika (Ardhi, Kilimo na Mifugo na Uvuvi) zishiriki kikamilifu kwenye zoezi hili na kila Wizara itenge bajeti ya kusaidia kupima ardhi na kushughulikia changamoto hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. OLIVER D. SUMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kwa kukushukuru kwa namna ambavyo umekuwa kiungo muhimu katika kuhakikisha Bunge letu tukufu linatimiza wajibu wake wa kuisimamia Serikali ili iweze kutimiza wajibu wake kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kupoteza muda ninaomba nianze moja kwa moja kutoa mchango wangu kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na mchango wangu unaanza kwa kuishauri Serikali kuwekeza nguvu kubwa katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa Maafisa Ardhi katika Wilaya zote na mikoa yote nchini ili waweze kupata ari na ubunifu wa kuweza kutimiza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi kirefu tumekuwa tukishuhudia migogoro mingi ya ardhi ambayo mara nyingi imetokana na Idara ya Ardhi na Mipango Miji katika maeneo mengi ya nchi hii kushindwa kutimiza majukumu yao kwa ufanisi kutokana na ufinyu wa bajeti na vitendea kazi katika Idara ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengi ningependa kuiomba Wizara ya Ardhi kuweka mpango wa matumizi bora ya ardhi katika maeneo yote yanayozunguka Hifadhi za Taifa nchini pamoja na maeneo yenye miradi ya kimkakati. Kwa kufanya hivyo itapunguza kwa kiasi kikubwa migogoro ya ardhi ambayo tumekuwa tukiishuhudia mara

kwa mara pale wananchi wanapoamua kuvamia maeneo ya mapori ama Hifadhi za Taifa kwa ajili ya kuendesha shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano Wilaya ya Ngara ambayo imepakana na Mapori ya Akiba ya Kimisi na Burigi kunahitajika kuwekwa mpango wa matumizi bora ya ardhi ili kuweza kuwanufaisha moja kwa moja wananchi wa Wilaya ya Ngara hususani wakazi wa vijiji vya Rusumo, Mshikamano, Kasulo, Rwakalebela, Keza na Kazingati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naiomba Wizara ya Ardhi kukaa pamoja na Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi kuandaa mpango huo wa matumizi bora ya ardhi ambao utahusisha kutenga baadhi ya maeneo kwa matumizi ya kilimo, ufugaji, uwekezaji viwanda pamoja na utunzaji wa mazingira kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ningependa kuishauri Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi kuandaa mpango bora wa matumizi ya ardhi hususani kwa Wilaya ya Ngara eneo la Mgodi wa Tembo Nickel. Kutenga maeneo matatu maalum kwa ajili ya shughuli za kiuchumi kama kilimo, ufagaji pamoja kuanzisha mpango wa kuinua hadhi ya Kijiji cha Bugarama kilicho eneo jirani ya mgodi huu ili kiweze kuwa na hadhi ya kibiashara.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Angelina Mabula (Mb) na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nampongeza pia Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete (Mb) na Naibu Waziri, Ndugu Allan Kijazi - Katibu Mkuu pamoja na Naibu wake Ndugu Nicodemus Mkapa kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maombi yafuatayo; kwanza kumaliza mgogoro wa *Lipalamba Game Reserve* na Kijiji cha Mseto kilichopo kata ya Lipalamba; pili, Wilaya ya Nyasa ni changa sana kimapato. Tunaomba mkopo ili kupima

maeneo ya fukwe yote na Mji wa Mbamba Bay ili usijengwe kiholela.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** *Mheshimiwa* Naibu *Spika*, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

*Mheshimiwa* Naibu *Spika*, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

*Mheshimiwa* Naibu *Spika*, napenda kumpongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa ustawi wa jamii na maendelo endelevu na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa ushindani wa kimataifa *(national competitiveness).* Bajeti hii inaenda sambamba na dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni *kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.*

*Mheshimiwa* Naibu *Spika*, naishukuru Serikali kwa kuanzisha mikopo inayotolewa kwa ajili ya kupanga, kupima na kumiikisha (KKK) ardhi. Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ni mnufaika wa programu hii na imekopeshwa shilingi 1,857,586,634. Mji Mdogo wa Mbalizi kumepimwa viwanja 35,000 kwa gharama ya shilingi 1,273,038,500 na Kijiji cha Mwashoma Kitongoji cha Inolo vimepimwa viwanja 565 kwa gharama ya shilingi 584,548,134 na umefanyika kwa ufanisi mkubwa sana. Kutokana mahitaji makubwa na faida

itayopatikana kwenye mauzo ya viwanja hivi, ipangiwe matumizi yanayolenga kuendeleza ardhi ikiwemo kuweka miundombinu kwenye maeneo yanayopimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mafanikio katika utekelezaji huu wa mwanzo, napendekeza Serikali iweke kipaumbele cha kuendeleza programu katika maeneo mengine hususani yanayolizunguka Jiji la Mbeya kutokana na mahitaji makubwa ya makazi yaliopimwa. Napendekeza Serikali iendeleze programu hii katika vijiji vya Swaya, Lupeta, Nsenga, Ifiga, Nsongwi Mantanji, Nsongwi Juu, Izumbwe, Iwindi, Igoma, Ilembo, Idimi na Haporoto. Upimaji kwenye vijiji unaharakisha kuwa miji *(growing towns)* utawezesha kupunguza na hata kuondoa kabisa makazi holela na pia kuongeza wigo wa walipa kodi.

*Mheshimiwa* Naibu *Spika,* pamoja na programu ya makazi, Serikali iweke usimamizi wa matumizi bora ya ardhi ya kilimo ambayo inaendelea kupotea kwa matumizi ya makazi. Katika kupangilia matumizi mazuri ya ardhi, ihusishe Wizara za Kilimo, Wizara za Maji na Wizara inayosimamia mazingira. Kwa vile binadamu tunaongezeka ni muhimu kuhakikisha ulinzi kwa kuhifadhi ardhi inayofaa kwa kilimo na pia kutenga ardhi kwa ajili ya wafugaji.

*Mheshimiwa* Naibu *Spika,* pamoja na hatua zinazochukuliwa na Serikali kurejesha mahusiano mazuri kati ya *TANAPA* (Hifadhi ya Kitulo) na wananchi wa Kata za Ilungu, Igoma, Ulenje na Inyala, bado suluhu haijapatikana. Kuna mgogoro wa miaka mingi wa mpaka kati ya *TFS* na wananchi wa Kijiji cha Mwashoma. Pia kuna mgogoro wa *TANAPA* (Hifadhi ya Kitulo) na wananchi wa Kijiji cha Kikondo ambao eneo lao lilichukuliwa na *TANAPA* bila kulipa fidia. Pamoja na changamoto hiyo ya *GN* za Hifadhi ya Kitulo, pia kuna utata wa mpaka wa Wilaya ya Mbeya na Wilaya ya Makete na inahitajika Wizara ya Ardhi kupitia upya mipaka na kurekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mgogoro huu kuchukua muda mrefu na kusabisha uvunjifu wa amani, kuna

ahadi ya mwaka 2015 alitoa Mheshimiwa Hayati Magufuli na kumwelekeza Waziri wa Ardhi wa wakati huo kupitia upya mipaka, ili wananchi wa Kijiji cha Kikondo waachiwe eneo leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nami niungane na Wajumbe wote au Wabunge wote kumpa salamu za pongezi sana Mheshimiwa Rais wetu Mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan mama maendeleo kwa zawadi kubwa au heshima kubwa ambayo imeendelea kutupa nchi kuhakikisha kwamba nchi ya Tanzania imeweza kufahamika katika usimamizi wa miradi lakini pia kwakipekee kabisa juu ya usimamizi wa fedha za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo pia nichukue nafasi hii kuwashukuru sana na kuwapongeza sana Wabunge wote waliochangia katika hoja ambayo imeletwa na Mheshimiwa Waziri wetu wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambayo kwa jumla au kwa rekodi tulizonazo waliochangia kwa mdomo walikuwa watu 27 na waliochangia kwa maandishi ni watu wawili. Binafsi yangu kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri niwashukuru sana Wajumbe wote kwa michango yao mizuri, lakini kabla sijaanza kujibu hoja ambazo zimeelezwa nataka nikuhakikishie na Bunge lako kwamba mawazo yote yaliyotolewa, ushauri wote sisi kama Wizara tunaichukua na tutakwenda kuyafanyia kazi ili kuhakikisha kwamba ardhi yetu au rasilimali ardhi yetu inakuwa salama na wananchi wetu wanaendelea kufaidi matunda ya kuwepo kwa Rais Samia Suluhu Hassan katika nchi hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutoa majibu haya nitajaribu kujibu kwa jumla. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe sitatumia nafasi hii kutaja majina ya mmoja mmoja, lakini

nadhani katika maelezo moja kati yenu mtakuwa mnajua kwamba hili jambo niliuliza na linatolewa majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika eneo la migogoro ya ardhi; nataka nitoe taarifa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri kwamba Serikali imekuwa inafanya hatua nyingi sana za kuhakikisha kwamba migogoro ya wakulima na wafugaji, migogoro baina ya vijiji vyetu, lakini migogoro juu ya matumizi ya ardhi yameendelea kushughulikiwa na katika kufanya hivyo Kamati ya Mawaziri Wanane imeendelea kufanyakazi kama ambavyo imeelezwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo pia yamefanyika mabadiliko ya sheria, lakini yapo maelekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais juu ya jinsi gani migogoro hii inakwenda kutatuliwa ili kwa wananchi amani na utulivu vipate kurudi katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo tumeendelea kufanya ziara za mara kwa mara; na katika kufanya hivyo migogoro mingi imetatuliwa lakini kwa kipekee kabisa nataka niwahakikishie ndugu wajumbe au Wabunge kwamba migogoro ile ambayo imetajwa katika mjadala wetu kwa mfano ule wa Efatha kule Rukwa, nataka nikuhakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba kilio chenu, sauti yenu imesikika si tu ndani ya Bunge lakini hata kwa wananchi wetu katika eneo la Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo ya Wizara yalishatolewa juu ya jinsi gani tunaweza tukautatua mgogoro ule lakini pia hatua za kimsingi juu ya utatuzi zilishafanyika lakini tunatambua kama Wizara kwamba zipo kesi ambazo zilifanyika lakini maamuzi yaliyofanyika ya mwisho ya mwaka 2018 ya kugawa maeneo kwaajili ya wananchi haya yanataka twende tukayasimamie ili yaweze kutatua mgogoro huo. Lakini pamoja na hilo nataka niwahakikishieni ndugu wajumbe mliotoa sauti yenu kwamba sisi kama Wizara tutafika baada ya Bunge hili na kubwa zaidi ni kuja kutatua kero hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia limezungumza jambo la Mbarali, nalo pia nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mtenga lakini pia dada yangu Mheshimiwa Bahati kwamba nalo tunalitambua Kamati ya Mawaziri imefika nako tutakwenda ili kwenda kukutana na wananchi tuzungumze ili tujue tunatatuaje si hilo tu pamoja na migogoro mingine yote katika eneo la nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu Wabunge nawashukuruni sana kwa mawazo wenu mazuri juu ya jinsi gani hii Wizara inaweza kuongeza makusanyo ya maduhuli, lakini pia nataka nikuhakikishieni kwamba zipo hatua za msingi ambazo Wizara imekuwa inazichukua kuhakikisha kwamba maduhuli yanakusanywa. Kwa mfano, katika hatua ambazo zimefanyika katika mwaka huu wa fedha ni pamoja na kuendelea na kazi ya kupanga na kupima kwa sababu utakapopanga na kupima maana yake tunakwenda kuzalisha hati ambazo hati zile zinaenda kututolea pesa na makusanyo yanakwenda kuhakikishiwa, lakini pamoja na hilo pia sasa tupo katika utaratibu wa kubadilisha mfumo wetu wa kidijitali ameeleza ndugu Kunambi jana juu ya umuhimu wa kuhakikisha kwamba ule mfumo *ILMIS* unatandazwa Tanzania nzima na ule mfumo utakapokuwa umetandazwa Tanzania nzima ndiyo tutakwenda kujihakikishia makusanyo yenye uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hilo tu pia ipo mifumo mbalimbali ambayo tunajaribu kui-*harmonize* pia ikiwa na mifumo mingine ya ukusanyaji wa maduhuli ikiwemo ya *TRA,* lakini pia kuangalia kama ipo mifumo mingine rafiki ambayo inaweza ikatusaidia katika kuhakikisha kwamba makusanyo yanahakikishiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo pia nataka kukuhakikishia kwamba tunaendelea kutoa elimu, si tu kwa wataalamu wetu lakini pia kwa wananchi kuelewa umuhimu wa kuwa na hati ili hati hizo zitakapokuwa zinalipiwa basi Serikali yao iendelee kukusanya maduhuli na kufikia malengo makubwa kama ambavyo tumesema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo kupitia wahisani mbalimbali fedha zimeendelea kukusanywa, lakini pia kupitia programu mbalimbali kwa mfano sasa hivi katika kipindi hiki cha Sensa ya Makazi tumeendelea pia kupima na kutambua nyumba zetu ikiwa ni moja ya hatua ya kuhakikisha kwamba tunazimbua nyumba hizo na ili tuweze kukusanya maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwashukuru ndugu wajumbe au ndugu Wabunge kwa mawazo yao mazuri na msukumo walionao kuhakikisha kwamba tuna-*harmonize* mipaka baina ya nchi yetu na nchi marafiki. Lakini nataka nikuhakikishieni pamoja na mawazo mazuri ipo miongozo toka Umoja wa Mataifa Afrika kwamba mpaka tunafika mwaka 2027 mipaka baina ya nchi zote zinazozungukana iwe imeweka vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie na Bunge lako kwamba Serikali yako chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan tunaendelea kufanyakazi kubwa ya kuhakikisha kwamba mipaka yetu inaendelea kuwa salama, lakini timu yetu ya watalaamu inaendelea kufanyakazi na watalaamu wa nchi marafiki au nchi majirani ili kuhakikisha kwamba mambo yote yanakaa vizuri na hivi karibuni ndugu Wabunge mnaweza mkawa mashahidi ujumbe wa watalaamu toka Kenya na Tanzania ulikutana kwa ajili ya kukuhakisha kwamba haya matatizo au changamoto zinazotokea katika eneo la mpaka wetu ikiwemo kule Jasini kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge nalo pia ni moja ya jambo ambalo tunaenda kulitatua.

Nataka kuwahakikishieni kwamba Serikali imetoa maelekezo na sisi ndani ya Wizara maelekezo hayo tumeendelea kuyasimamia na wataalamu wetu wapo *site* kuhakikisha kwamba jambo hili linatatulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wamezungumzia juu ya tatizo ambalo Wabunge wanalipata juu ya usalama wa mazingira yetu haya tunayofanyia kazi hasa ukizingatia eneo la Bunge ni dogo, lakini pia usalama

wa maisha yetu hasa tunapovuka barabara na matumizi ya vyombo vyetu tunapotoka Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba jambo hili linakaa vizuri Ofisi yako ya Bunge iliandikia Ofisi yetu na mbele ya Bunge hili nikiri kwamba Wizara yetu imepokea barua yenu na kuifanyia kazi na hapo ninapozungumza katika viwanja 13 ambavyo vinaonekana vilivyo pembeni ya eneo la Bunge viwanja 11 vimekwishafanyiwa tathimini na *value* yake imekwishajulikana, lakini pia tutakapokuwa tumemaliza viwili vilivyobakia tutaleta ile taarifa kwa mamlaka husika ambaye ni Katibu wa Bunge ili sasa mchakato uweze kufanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, angalizo; katika sheria yetu Sura Namba 118 ya Utwaaji wa Ardhi na Sura Namba 113 ya Ardhi inatuelekeza kwamba unapotaka kutoa ardhi mamlaka husika lazima ihusishwe; hivyo, nataka nitoe angalizo kwetu kwamba pamoja na kwamba utaratibu unaendelea, lakini mamlaka husika ambayo kwa mujibu wa sheria na Mheshimiwa Rais basi naye lazima tumuhusishe katika jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka nirejee angalizo alilolitoa au rai iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wakati anatoa hotuba yake juu ya kuhakikisha kwamba riba au hizo *interest* za maeneo au hela zinazotakiwa zilipiwe katika utoaji wa maeneo zinafanyika mapema ili kuepusha usumbufu wa kulipiana fidia na riba zingine zisizofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka nizungumzie jambo la Mabaraza ya Ardhi; nikurejeshe katika Mabadiliko Madogo ya Sheria Sura Namba 216 yaliyofanywa katika Sheria Ndogo Namba Mbili ya mwaka 2021 ambapo baadhi ya mambo makubwa yanayokwamisha utolewaji wa haki yalifanyika. Moja ya mabadiliko hayo ilikuwa ni kuhakikisha kwamba wenyeviti wetu wa Mabaraza ya Ardhi sasa wanakuwa ni waajiriwa na si vibarua au watu wanaojitolea kama ilivyokuwa mwanzo na katika kufanya hivyo mafanikio yameonekana sasa; mafanikio yameonekana kwa sababu

waliopo ni kwamba wanakataa rushwa kwa vitendo, lakini kwa wale wachache ambao wameendelea kupokea rushwa nataka nikuhakikishie wizara yako, Serikali yako inaendelea kutoa macho katika hao wasio waadilifu na tutaendelea kuwashughulikia kadri ambavyo tutakwenda kupata malalamiko toka kwa wananchi wetu ambao wanalalamika haki kutotendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hilo katika mabadiliko hayo ambayo yamefanyika sasa, moja ya jambo kubwa ambalo limefanyika ni kuhakikisha kwamba mamlaka yale ya kuamua juu ya kesi nayo pia yamebadilika, Mabaraza yetu ya Kata na Vijiji yamebakia na kazi ya usuluhishi tu, lakini Mabaraza kuanzia Wilaya ndiyo yanaopenda kuamua *on issue of meriting,* huku chini wanaamua katika mambo ya mahusiano tu, yaani katika maana kwamba kuwapatanisha wananchi na siyo kuleta mgongano ambao utakuja kutusumbua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuakikishie Bunge lako kwamba katika mwaka wa fedha uliopita Wizara yetu ya Ardhi imeweza kufungua Mabaraza mapya 20 ikiwa ni sehemu ya kuongeza mkazo wa kuhakikisha kwamba haki inawakaribia wananchi na kuwafikia na katika mwaka huu wa fedha Bunge lako litakapotupitishia mafungu yetu tunakwenda kumalizia Mabaraza 59 yaliyobakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu sahihi na mazuri. Mheshimiwa mtoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge nianze kwa kumshukuru Mungu kwa fursa ambayo ametupa hadi tunafikia hatua hii tunapokwenda kuhitimisha hoja yetu. *(Makofi)*

Aidha, niungane pia na Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Mama Samia Suluhu kwa tuzo aliyoipata. Naomba niishie hapo kwa sababu pongezi nyingi zimetolewa lakini nia na dhamira ya dhati sana ni kwamba kuhakikisha watanzania kwamba tunaye Rais ambaye anafanya kazi na kazi hiyo inatambulika katika ulimwengu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge 27 waliochangia kwa kuzungumza na Wabunge wawili wamechangia kwa maandishi, kwa sababu hoja ni nyingi na nyingi zinahitaji maelezo ya msingi ili muweze kuzielewa vizuri tutaleta pia kitabu ambacho kitakuwa kinaelezea hoja moja baada ya nyingine. *(Makofi)*

Kwa hiyo kwa nafasi hii niliyopewa ya dakika 20 nitakwenda kujibu hoja chache ambazo zinahitaji maelezo ili tuweze kuona jinsi gani tunafahamisha kikao chako hiki cha Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliyopigiwa kelele sana na Waheshimiwa Wabunge hasa ile pia ya Mawaziri Wanane katika vile vijiji 975. Kama nilivyosema kwenye hotuba yangu tunastahili sana kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu vijiji vile 975 angekuwa ni Rais ambaye si msikivu asingeridhia vijiji 920 kuweza kuridhiwa na kurasimishwa na kupewa watu na tukumbuke katika changamoto hiyo ambayo ipo maeneo mengi ambayo yana migogoro kuna muingiliano wa matumizi ya ardhi unakuta kuna maeneo ambayo yalitengwa kwa ajili ya hifadhi lakini kutokana na sababu pengine ziwezi kusema zilisababishwa na nini tukajikuta tena tumeingia katika mgogoro mwingine wakuhalalisha vijiji ndani ya maeneo ambayo tayari yanahifadhi. Kwa hiyo, hapo ndipo mgogoro ulipoanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika utatuzi maelekezo ndani ya Serikali ni kwamba lazima tuangalie vijiji ambavyo havina athari viweze kurasimishwa lakini tukumbe katika vijiji hivi 920 vinarasimishwa, vinavyobaki 55 shughuli inaendelea ya kufanyia tathimini. Tukumbuke katika hivi vijiji

55 tunayo miradi mikubwa ya kimkakati ambayo iko kwenye maeneo hayo, nikichukulia mfano wa Bwawa la Mwalimu Nyerere wote lazima tujiulize hivi lile bwawa kama halitaweza kupata maji ya kutosha na pesa yote iliyowekezwa pale maana yake Serikali itakuwa imepoteza fedha nyingi kwa ajili ya kutengeneza lile bwawa ambalo mwisho wa siku litakuwa halifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini maeneo yale yamezungukwa na watu ambao wanafanya kazi katika vyanzo vya maji ambavyo vinazuia maji kwenda katika ule mkondo ambao unapelekwa kwenye bwawa. Kwa hiyo, Serikali imejikita katika kufanya tathimini ya kina athari ambazo zinaweza kusababishwa na watu kuwepo na shughuli za kibinadamu na wakati huo huo bwawa linategemea maji yale.

Kwa hiyo, kinachofanyika pamoja na Mawaziri Wanane kwenda kazi ya mikoa, lakini tukumbuke ile mikao saba au nane ya mwanzo Kamati ile inakwenda kwenye vijiji inaongea na wananchi na baadaye inakuja inawaachia mkoa kwendelea na hile shughuli na timu ya wataalamu inabaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukihesabu vijiji hivyo kama ngazi ya Taifa peke yake ndiyo itakuwa inakwenda kwenye maeneo, hiki tunachokipigia kelele cha migogoro itachelewa kutatuliwa kwa sababu siyo rahisi ngazi ya Taifa kwenda vijiji vyote na ukamaliza, tunaachia mamlaka ya mkoa, wanaofahamu maeneo yao, wanaoweza kuzungumza na watu pale na ambapo hata sisi tumeshatoa maelekezo.

Kwa hiyo tunachofanya kama Serikali ni kuwataka mamlaka zilizoko kwenye maeneo ambayo bado yanafanyiwa tathimini kuweza kuangalia uhalisia wakisaidiwa na wataalamu wetu, uhalisia wa maeneo yale yaachwe kama yalivyo, wananchi waendelee kufanya shughuli zao au kuna haja ya kuwaondoa wananchi maeneo yale ili miradi ile iwe salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hiyo tathimini yake bado inaendelea, kwa hiyo, mpaka sasa hapa ninapozungumza siwezi kukwambia nani na nani ataondoka pale ni mpaka ile tathimini ikamilike na wataalamu wapo. Na mimi niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, pesa nyingi mnahidhinisha kwa ajili ya miradi ya kitaifa, sasa tukiidhinisha pesa halafu sisi wenyewe tukataka kukwamisha mwisho wa siku tutakuwa tunapoteza nguvu ya umma lakini tutakuwa tunapoteza pesa ya Serikali kwa kukwamisha miradi ambayo tunajua kabisa ni vielelezo kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi niwaombe katika hivyo vijiji ambavyo tathimini inaendelea muwaamini viongozi wenu ndani ya mkoa, muwaamini viongozi wenu ndani ya Serikali hakuna utatuzi utakaokwenda kufanyika bila kushirikisha wananchi, wananchi watashirikishwa sehemu zote na maelekezo ya Serikali ndivyo yalivyo.

Kwa hiyo, tulikuwa tunakwenda kwa ajili ya kutoa maelekezo naomba sana hili lieleweke kwa sababu limechukua kidogo wazungumzaji wanaotoka katika maeneo hayo wamezungumza sana. Ikiwemo na *GN* 28 ambayo ni kati ya yale ambayo yanakwenda kufanyiwa kazi ukanda huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumzwa hapa suala la fidia, suala la fidia limekuwa ni changamoto na kizungumkuti katika maeneo mengi. Tunazo taasisi nyingi zinazodaiwa, Waheshimiwa Wabunge hapa wametaja baadhi, wametaja maeneo ambayo yamechukuliwa kwa muda mrefu na wengine wanasema karibu miaka 20, 25 lakini fidia hailipwi na tayari watu pale wanaathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke mwaka 2017 tulipitisha sheria hapa tukaipitia ile Sheria ya Fidia ambayo ilikuwa haina muda maalumu ambayo ilikuwa inaonesha kwamba watu wakitaka kutwaa eneo kama hajalipa fidia ndani ya muda kadhaa aweze kuendelea mwananchi na shughuli yake. Tulipitisha hapa kwamba ni ndani ya miaka miwili kama mlipa fidia hajalipa mwananchi anaendelea na

shughuli yake, lakini hiyo ilikuwa yale maeneo ambayo yametwaliwa kwa sasa na kila baada ya miezi sita anakuwa *charged* na *interest* kama hatalipa.

Kwa hiyo, mimi niwatake mashirika yote na taasisi zote pamoja na wawekezaji ambao wanachukua maeneo ya wananchi kulipa fidia kwa wakati, vinginevyo Serikali haitakubali na hata kwenye hotuba yangu nimesema kama taasisi ya ushirika haijajiandaa katika kulipa fidia wasichukue maeneo ya watu, hilo ndiyo tunalolizungumza kwa sababu tunaleta kero ndani ya Serikali lakini unapotaka kufanya mradi lazima uwe umejiandaa kuhakikisha kwamba utalipa fidia hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo yaliyotajwa ya *EPZA* tayari Serikali imeshaanza kuyachukua baadhi ya maeneo ili mengine yanagaiwa wananchi, lakini pia nitoe tahadhari kule ambako maeneo yanarejeshwa tuweze kuweka mpango mzuri wa matumizi ili basi ardhi ili itufae katika matumizi. Kwa mfano maeneo ambayo yanakuwa yana mashamba, Wabunge wengi mmeomba mashamba wametaja Mbunge wa Mkinga kule ametaja na wengine wametaja kwamba kuna maeneo ambayo yapo tu yamekaa likiwepo shamba la Efatha limetajwa kwamba halijaendelezwa.

Naomba niseme ya kwamba maeneo ambayo yanaumiliki sahihi wa kisheria, taratibu zile za kuyatwaa lazima zizingatiwe. Kwa hiyo, inapofikia mwisho anayekwenda kubatilisha umiliki huo ni Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, ikienda kwa Mheshimiwa Rais na Waziri akimshauri Mheshimiwa Rais kubatilisha kama Mheshimiwa Rais akiona hii inafaa atafanya na kama alivyofanya na mpaka na kufuta yale mapori 12 ambayo wananchi wamepangiwa.

Kwa hiyo katika ufutaji au katika utwaaji lazima sheria zinafatwa. Kuna maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wanalalamikia kwamba yamekaa *idle* na watu hawaendelezi lakini ukiangalia taratibu za kuanza kufuta ukienda kwenye Sheria Na. 4 ukianzia kile kifungu cha 45

unakwenda mpaka kifungu cha 48 kuna taratibu zote zimewekwa. Kuna kumpa onyo akajibu, kuna kumwambia ajirekebishe, kuna kumpa *notice* yakumnyang'anya. Sasa usipofuata taratibu zile huku Wizarani hatuwezi kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Rais kufuta, lazima taratibu zifatwe na wengine wanatoa Ilani halafu wanatulia, sasa sisi huku Wizarani au Serikalini hatuwezi kuja kukupangia wewe nani anyang'anywe wewe uliyekaa kule ndiyo Mamlaka za Upangaji wa Miji, angalia taratibu zako zote kisheria zimezingatiwa, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, kuna mengine yanakuwa yana migogoro kwenye Mahakama mfano mzuri shamba la Efatha linalozungumziwa, Serikali na Mheshimiwa Naibu Waziri amelijibu pale. Lakini Serikali ilishafanya kazi yake vizuri na Mahakama ikatimizwa wajibu wake na hii ni Mihimili mitatu iliyo tofuati. Kama kuna agizo la Mahamaka sisi hatuwezi kuliingilia kwa sababu tunaheshimu ule Muhimili. Lakini bado tulifanya mazungumzo na wenzetu wa Efatha na wakaridhia ekari 3,000 kutoka kwa ajili ya kugawia vile vijiji vitatu vinavyozunguka pale.

Kwa hiyo kazi inayotakiwa kufanyika pale ni zile ekari 1,000 waweze kuonyeshwa. Lakini utaratibu wa kusema unamnyang'anya kwa sababu tayari shamba lile lilipata nadhani hati yake kwenye mwaka 1997, kijiji au vijiji vimekuja kuandikishwa mwaka 2007 vimeandikishwa ndani ya umiliki wa muhusika. Sasa pale inakuwa ni vigumu vinakinzana katika namna vyote vimetoka Serikalini halafu wananchi wanabaki wanaangalia. Lakini kwa kuona tatizo hilo ambalo tayari lilionekana ndiyo maana Serikali ilichukua uamuzi wa kuzungumza naye ili aweze kuridhia ekari 3,000 zitolewe wananchi wapewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hii inakuwepo kwa sababu tu namna ambavyo tunaishi kule katika maeneo na wawekezaji na namna ambavyo wawekezaji wasivyokuwa waaminifu katika kutimiza masharti ya hati wanazozimiliki. Kwa hiyo, ndiyo changamoto kubwa ambayo sasa Wizara yangu itaendelea kuangalia kwa kina na naagiza

katika kikao hiki Halmashauri ambazo ni Mamlaka za Upangaji fanyeni ukaguzi wa maeneo yote ambayo wawekezaji wamepewa na muangalia masharti yake kama yametimizwa kama hayajatimizwa taratibu za kuwanyang'anya zianze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tutakapokuwa tumewanyang'anya kwa mfano kwenye mashamba tusikimbilie kupanga viwanja, kuna maeneo wanataka kwa ajili ya kupanga tukipanga viwanja maana yake tutajikuta tunakosa hata maeneo ya kilimo. Kilimo cha mjini kinakubalika, kwa hiyo chukua eneo, panga maeneo yako kama yameshavamiwa na watu tutapanga makazi ambayo hayajavamiwa basi wekeni kile kilimo cha mjini ili walau wananchi waweze kupata maeneo ya kuendelea kuwa na kilimo. Sasa leo ukimnyang'anya mmiliki aliyekuwa analima, halafu wewe ukaweka majengo tu maana yake utakuwa hujaisaidia Serikali. Kwa hiyo, naomba kusema kwamba taratibu zizingatiwe na tuone jinsi ambavyo tunafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mheshimiwa Mwita Waitara ambalo amelizungumzia eneo lake ambalo amelisema la Kijiji cha Komarero ambalo lina jumla ya ekari 652 tayari katika eneo lile lina wananchi 6,847 tathmini ilishafanyika na fidia imeshalipwa kwa watu 1,515 kati ya hao 6,847. Na katika kijiji kingine ambacho amekitaja cha Kewanja tayari kazi ya tathmini inaendelea kule, tatizo linalokuja ni katika lile eneo ambalo mwekezaji alitaka kulichukua akiwa na mawazo ya kuwa na ile *open pitch process* za kuchimba, baadae akabadilisha mawazo akasema anakwenda kwenye *underground,* akaamua kuacha.

Serikali hatujakaa kimya tumefanya mazungumzo naye ili aone namna gani, kwa sababu wananchi wale walisimama kwa muda mrefu kuweza kuendeleza maeneo yao kwa sababu alionesha nia ya kulichukua. Lakini kashindwa kulichukua pengine kwa sababu amebadilisha, badala ya kuwa na *open pitch* sasa anakwenda na *underground* kwenye uchimbaji wa madini.

Kwa hiyo, tumemtaka pengine aweze kuona namna ya kulipa walau fidia kidogo kwa wale aliowachelewesha, lile amelichukua na amepeleka kwa mshauri wake anasubiri kushauriwa namna ya ambavyo ataweza kuwalipa kwa sababu kosa ni la kwake na siyo la wananchi amewachelewesha katika maendeleo yao. Kwa hiyo, hayo yote yanafanyika kwa kuangalia ni namna gani tunaweza kusuluhisha haya mambo yaweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamezungumzia suala la kupanga, kupima na kumilikisha na hiyo ndiyo hoja ya msingi zaidi pengine ningetaka Waheshimiwa Wabunge tuichukue vizuri na tuone namna gani tunafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yetu ni Wizara ambayo inasimamia, inatunga sera, Miongozo mbalimbali kwa ajili ya kusimamia katika taaluma yake au sekta ambayo inaiongoza. Mamlaka za Upangaji zote ni Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Namba 8 ya Mipango Miji ya mwaka 2007. Takwa hili la kisheria si mamlaka zote za Halmashauri zinalitekeleza Serikali imeingilia kati kutaka kuongeza ile kasi pengine ya upimaji ili kupunguza malalamiko ya wananchi na ndiyo maana Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan tunamshukuru sana kwa kutoa ile shilingi bilioni 50 ambayo tumekwenda kuikopesha katika Halmashauri 55 lakini kuna pesa nyingine ambayo imetoka bilioni tano ambayo imekwenda kufanya kazi ile ile. Lengo letu ni kutaka kusaidia kusukuma kwenye mamlaka husika ambayo ndiyo hasa inayotakiwa kufanya kazi ya upangaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya Wizara kusaidia mamlaka zote zimetulia kama vile ile ni kazi ya Wizara. Mkitulia na kuachia Wizara maana yake ni kwamba tutachelewesha wananchi kuweza kupata umiliki ya maeneo yao na kuwajengea uwezo kiuchumi. Ninyi wenyewe hapa mmesema sekta ya ardhi ni sekta ambayo tukiweza kuisimamia vizuri itakwenda kunyanyua uchumi wa kila Mtanzania. Lakini tunaisimamiaje kama hatuwezi kuwamilikisha wananchi na kuwapa uwezo wa kutumia miliki zao kwenda kukopa benki.

Kwa hiyo niwatake sana Mamlaka za Upangaji watimize takwa lao la Kisheria sisi kama Wizara tutaendelea na ule mfuko ambao tulikuwa tukiutumia katika kukopesha bado tumeendelea kumuomba Mheshimiwa Rais kwamba tuweze kurejeshwa ili tuongeze ile nguvu ambayo tunaweza kusaidia. Rai yangu kwa Halmashauri zinapewa pesa Wakurugenzi wanatumia tofauti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ni sehemu ya Baraza la Madiwani mnapokuwa kwenye vikao watakeni Halmashauri zenu wawaoneshe matumizi ya pesa waliyopewa kwa ajili kupanga, kupima na kumilikisha ili tuweze kuona ile kasi tunaenda pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo tunawataka pia kumekuwa na changamoto pengine ya pesa tunasema wanapouza wanakuwa na pesa nyingi za kutosha, basi katika zile pesa wanazozipata waweze kugawa kulingana na madaraja ya Halmashauri zetu. Watenge kati ya asilimia 40 mpaka 60 ya pesa zile wanazozipata faida kwenye mauzo zikaendeleze sekta ya ardhi badala ya kuzitumia kwenye matumizi mengine. Tukifanya hivyo tutajikuta kasi imeongezeka na tunatambua sana katika suala hili kama Halmashauri zingeweza kutenga walau vijiji au hasa vijiji vitano, 10 kila mwaka tungeweza kusogea mbele. Lakini hawafanyi kazi hiyo wanaangalia Tume, Tume iko kwa ajili ya kuwezesha katika kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo Tume inaingia pia katika suala zima la kupanga mpango mzima wa matumizi ya ardhi ikiwa pia ni kuhakikisha Halmashauri zinajengewa uwezo kupitia zile Kamati zake waweze kuendelea na hili zoezi.

Kwa hiyo, mimi niwaombe Halmashauri waone kwamba hili pia ni jambo la msingi kama Serikali tunatakiwa kulifanya kwa pamoja ili tuweze kuona tunakwenda namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika masuala mengi ambayo yamezungumzwa limezungumzwa suala la hatimiliki za kimila kuweza kukopa benki. Naomba niseme tu kwamba tunao mfano mzuri Halmashauri ya Mbinga, Bariadi, Babati

na nyinginezo ambazo zimetumia hatimiliki za kimila kuweza kukopa benki, tatizo lililopo tu hapa ni la kisheria ambalo kama Mheshimiwa Kakunda alivyosema tutakwenda kuiangalia sheria. Kwa sababu hairuhusu mtu mmoja anapojisikia kwenda kupima aende apime, lazima mamlaka zinazohusika ziweze kufanya kazi hiyo.

Kwa hiyo tutaiangalia ile sheria tuweze kuona ni jinsi gani tunaweza tukaweka utaratibu ambao utaongeza kasi ya kumiliki, kwa sababu sasa hivi mtu akitaka kupima anaambiwa pengine apime na wanakijiji wenziwe wote kitu ambacho kinakuwa ni gharama ambacho pengine yeye hawezi. Lakini kama Halmashauri zetu zingefanya kazi hiyo zingeweza kutusaidia sana. Kwa hiyo mimi niombe tu hayo yaweze kufanyika ili tuweze kuona ni jinsi gani tunakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la uwekezaji limezungumzwa hapa Mheshimiwa Chumi amezungumza na nimpongeze kwa kutenga eneo la *industrial park* sisi kama Wizara tayari tumeshatenga hekta 224,000 tukiwa tumejiweka tayari kwa sababu tunafahamu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan ameshatuelekeza, Wizara iwe tayari wawekezaji wanapoingia maeneo yawepo. Niwaombe tena Mamlaka za Upangaji, Mamlaka ambazo zimeshaandaa mipango kabambe kwa ajili kutenga maeneo kwa matumizi hakikisheni maeneo yale yanakuwa na umiliki *either* imilikiwe na Halmashauri au imilikiwe na Halmashauri ya Kijiji au Halmashauri yenyewe kwa maana ya kwamba mwekezaji anapopatikana asianze tena kusubiri mchakato wa uhaulishaji kama ni eneo la kijijini, lakini kama ni la mjini basi tujue umiliki uko kwa nani ili mwekezaji anapokuja anakwenda moja kwa moja tayari kwa mmiliki na wanakubaliana namna ya kulitoa lile eneo. Mwekezaji akija mpaka twende kijijini tuweke vikao tunachelewesha kitu ambacho Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan hataki kusia hayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo mimi niwaombe sana katika hili Mamlaka za Upangaji zione haja ya kuona ni jinsi gani tatakwenda kutatua tatizo hili kwa sababu tunajua ni hitaji nchi

imefunguka na wanahitaji kuwa na wawekezaji wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine nitayaruka lakini nizungumzie suala la *National Housing*; limezungumzwa suala la nyumba zimechoka ni kweli nyumba nyingi, lakini tukumbuke mwaka jana tuliripoti hapa walikuwa wameshaweka mpango kwa ajili ya kufanya ukarabati na walitenga shilingi bilioni nane kwa ajili ya kuendelea kufanya ukarabati katika majengo yao 300 ambayo hasa yapo katika Mkoa ya Kilimanjaro, Mtwara, Katavi na Tabora itaingia katika mwaka huu wa fedha. Ni kweli yako yamechoka, lakini tunaamini, mmempongeza pia na Mkurugenzi Mkuu ninaimani kwa usimamizi wake atakwenda kufanya kazi yake vizuri. Na majengo yale ya uwekezaji ambayo yamezungumzwa yalikuwa yamesimama kwa muda mrefu tayari Serikali ilisharidhia ili waweze kuendelea kuyakwamua na kuendelea kuweza kuendelea nayo kama kitega uchumi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tusema haya yote tunayachukua tukitambua ya kwamba tupo pamoja katika kuhakikisha kwamba kila ambalo mnaelekeza, kila ambalo mnashauri tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Utalii wameelekeza mambo mengi ushauri wao wameutoa tumeupokea kwa jinsi walivyoutoa, lakini niwahakikishie tu siku zote tumekuwa tuko pamoja katika hili. Tuzungumzie suala la kutofikia malengo katika ukusanyaji, kama ambavyo *property tax* iliingia kwa watoaji huduma sisi Wizara tunataka pia kuzungumza na watoa huduma kama wa maji ama *TANESCO*. Mtu ambaye anayetakiwa kulipa kodi pengine ya 300,000 kwa mwaka ukiagawa kwa miezi 12 utasikia ni kidogo sana.

Kwa hiyo, tunajaribu kuangalia namna itakavyokuwa mbali na hiki ambacho amekizungumza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba ile mifumo yetu pia itakwenda kuongeza kasi ya makusanyo. Lengo la Serikali ni kuhakikisha tunawezesha

mfuko mkuu wa Serikali kupata kile ambacho Mheshimiwa anakihitaji. Tusipo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa toa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Umejibu vizuri sana, toa hoja. *(Makofi/ Kicheko)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba tumeyachukua, tutayafanyia kazi, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namuita *Right Honorable Dr. Tulia Ackson*, Spika wa Bunge la Tanzania, kukamilisha hatua inayofuata. *(Makofi)*

*Hapa Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikali Kiti*

**SPIKA:** Katibu!

**NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Kamati ya matumizi.

Waheshimiwa Wabunge, tukae katibu!

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitabu cha Pili, Fungu 48 ukurasa wa 308.

**Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.......Sh. 11,530,075,294

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina mshahara wa Waziri na wapo Waheshimiwa Wabunge ambao ninayo majina yao hapa wanaotaka ufafanuzi wa jambo mahsusi la kisera.

Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Wakati nimepata fursa ya kuchangia hapa ningependa kujua kwamba katika eneo la Jimbo la Tarime Vijijini hasa kwenye eneo la fidia ya maeneo ya Mgodi *Barrick North Mara* kumekuwa na madai ya muda mrefu ya malalamiko yetu mengine toka mwaka 2012 mpaka sasa na watu wetu wameshindwa kuendeleza maeneo yale hawajalipwa fidia kwa hiyo hawajielewi wafanye nini.

Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze au aeleze Bunge hili ni kwa namna gani ambavyo wamejipanga kumaliza migogoro hii na watu wetu waweze kujiendeleza kiuchumi na kimaisha? Na kama sitaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri naomba nitoe shilingi ili Waheshimiwa Wabunge wapate nafasi ya kujadili jambo hili kwa upana. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni yetu inayohusu kutaka ufafanuzi kwenye mshahara wa Waziri unataka uombe ufafanuzi wa jambo mahsusi la kisera. Sasa hili ni jambo mahsusi ndiyo, lakini siyo la kisera, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri mmeisikia hoja ya Mheshimiwa Mbunge, alichangia, lakini pia amesimama

hapa kuonesha kwamba bado kuna changamoto kubwa kwenye hilo eneo lake la uwakilishi. Kwa hiyo, mtumie utaratibu wenu wa kawaida wa kushughulikia jambo hilo ili wananchi wa Tarime Vijijini waweze kupata majibu ya hizo hoja zao.

Waheshimiwa Wabunge, Mbunge mwingine anayetaka ufafanuzi kwenye mshahara wa Waziri ni Mheshimiwa Halima Mdee. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo ya Taifa 2021/2022 mpaka 2024/2025 pamoja na mambo mengine iliekeza ndani ya miaka mitano tuwe tumepanga vijiji 6,160 kati ya vijiji 12,312 yaani tumalize *50 percent* ya vijiji ndani ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza sasa asilimia 75 ya ardhi ya mijini haijapangwa na ni muhimu vilevile Mheshimiwa Waziri akafahamu kwamba kupima viwanja, maana niliona anazungumza kuhusiana na kupima viwanja na kupanga matumizi ya ardhi ni vitu viwili tofauti. Wabunge walivyokuwa wakichangia na yeye mwenyewe kwenye hotuba yake amezungumza juu ya migogoro ya ardhi tusipopanga matumizi, tukajua wapi wakulima wanakaa, wapi wafugaji wanakaa, wapi uchimbaji wa madini tunafanya, wapi Hifadhi ya Taifa, tutapima viwanja viwanja kienyeji. Sasa sisi kama viongozi tuna jukumu la kuandaa Tanzania ya kesho, hatutaki Rais ajaye wa Tanzania azungumzie tena migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana leo na nisipojibiwa nitashika shilingi Kamati yako imesema kwamba hili jambo ndani ya miaka mitano tutimize nusu ya vijiji kila mwaka tunahitaji shilingi bilioni 10. Mwaka huu Tume ya Mipango imepewa shilingi bilioni 1.4, na hii taarifa siyo hii ni taarifa ya Kamati iliyosomwa mwezi Februari, tukapitisha azimio hapa shida ni hii hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna bahati Spika wetu wewe ni kijana, una *future* pana, tunaomba Serikali iji-*commit*

ama ulipeleke suala hili Kamati ya Bajeti tukaitafute hii shilingi bilioni tisa tumalize ili mwaka ujao tukija tusiambiwe mawaziri wamekwenda kuzurura huko kutatua migogoro. Tuambiwe Tume ya Mipango imepewa fedha, Tume ya Mipango imeongezewa rasilimali watu, ikashirikiane na Halmashauri zetu tupange. Mheshimiwa Waziri unajua Halmashauri zetu ni maskini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima sekunde 30, kengele imeshagonga.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nisipojibiwa nitatoa shilingi, ninaomba *commitment* ya Serikali ama maelekezo yako tukatafute hii shilingi bilioni tisa, hizi fedha ni kidogo, ni aibu. Tunatumia misuli kujadili.... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuweza kujibu swali la Mheshimiwa Mdee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi anachokisema ni sahihi kwamba katika suala zima ukitaka kumaliza migogoro na namna ambavyo Serikali pengine tutatakiwa kufanya ni kuhakikisha ardhi yote imepimwa na imepangwa ikawekewa matumizi ili kuondokana na migogoro.

Katika hili ambacho Serikali inafanya pamoja na kwamba Tume ya Taifa ya Mpango wa Matumizi haijapewa fedha ya kutosha kulingana na namna ambavyo hitajio lipo kubwa; lakini kama Wizara bado tuna ile mikopo ambayo tumesaini juzi ya kiasi cha dola milioni 150 ambazo kuna sehemu inakwenda kugusa Wilaya 40, ambazo zitakwenda kuwekewa mpango wa matumizi bora ya ardhi. Katika hilo tumepanga kufikia maeneo 50 kila mwaka.

Kwa hiyo, katika hii fedha ambayo ipo tunaanza na hii ambayo tuko nayo mkononi lakini tayari tulikwishaanza

mazungumzo na Wizara ya Fedha kuweza kuona ni namna gani pengine kasi ile itaongezeka kuweza kufikia lile lengo la maeneo 6,160. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuhakikishie tu Mheshimiwa Halima hoja yako ni ya msingi, lakini kama Serikali tumeliona na tayari tupo kwenye mazungumzo nadhani Waziri wa Fedha takapozungumza atatoa maelekezo ya ziada, lakini tayari mpango upo na tunaendelea nao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anazungumza mikopo, anazungumza kitu ambacho hatuna, kitu ambacho hatujui kama kitakuja. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa Mheshimiwa Halima Mdee, ngoja, ngoja, ngoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja Mweyekiti wa kikao ili Wabunge wenzangu wajadili hii hoja muhimu na ninajua sababu kila mmoja anakuwa analilia migogoro....

**MWENYEKITI:** Sasa ngoja kwanza ndiyo maana wakati mwingine mnachanganya mambo halafu Kiti kikifanya maamuzi hapa mtaanza kulalamika. Toa hoja nione watu kama wanakuunga mkono au hapana ukiendelea na maelezo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Katibu wapo wangapi hao waliosimama. Ahaa, Wabunge 10 kuna mwingine ameibukia sehemu.

Sawa Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Hoja ya Mheshimiwa Mdee imeungwa mkono; sasa

wengine wote tukae, wabaki wamesimama wanaoomba kuchangia hoja hii.

Katibu hebu ushike kalamu, haya Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Kandege, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Kilumbe, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Salome Makamba.

Haya naomba hiyo karatasi. Mheshimiwa Salome Makamba. (*Makofi/Kicheko)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi napenda niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Halima James Mdee kuhusiana na suala la upimaji na upangaji wa ardhi kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mimi natoka eneo ambalo lina wakulima na wafugaji na eneo ambalo lina hifadhi na mapori makubwa ambayo yamewekwa kwa ajili ya uhifadhi. Tusipopeleka fedha ya kutosha kwa ajili kupanga ardhi yetu kwa ujumla; eneo la kusema kwamba tunapima na kutoa hati peke yake ni *segment* ndogo tu kwenye *demand* kubwa kwenye nchi hii ya kupanga ardhi kwa ajili ya matumizi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu hivi karibuni tunaona migogoro ya wakulima na wafugaji, watu wanauwana kwa sababu ya kutokujua mipaka yao kwenye ardhi. Unafahamu tuna migogoro mikubwa kati ya hifadhi na watu ambao wanafuga; kila siku mapori tengefu yanaongezeka, haijulikani mipaka na kwa bahati mbaya mfugaji mfugo wake ukiingia kwenye hifadhi yeye unataifishwa; lakini mfugaji akijeruhiwa na wanyama inaonekana yeye ndiyo amevamia mapori.

Mimi naiona *demand* kubwa na kama anavyosema Mheshimiwa Mdee hatuwezi kutegemea fedha ya mkopo ambayo hatujui kama itakuja au haitakuja. Njia pekee ambayo tunayo, Mheshimiwa Waziri ipo fursa ya kupeleka

jambo hili kwenye Kamati ya Bajeti na ndiyo maana zamani bajeti za wizara zilikuwa zinakuja baada ya kusomwa Bajeti Kuu. Lakini imebadilishwa sasa hivi tunasoma bajeti za Wizara kwanza halafu ndiyo inakuja Bajeti Kuu ili kuruhusu *adjustment* kama fedha yoyote, kuna mahali popote jambo halikupangwa vizuri liweze kupangwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naiona haja na ipo sababu na tuna kila sababu na tuna kila sababu sisi kama Wabunge tunaoshauri kulichukua jambo hili na kulipeleka Kamati ya Bajeti ili liende likafikiriwe upya, liende likapangiwe fedha, wananchi waweze kufahamu mipaka yao, haki zao na wajibu wao kwenye ardhi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako, mimi nakuomba tukubaliane na suala la kulirudia suala hili la ku-*review* bajeti ya Tume hii ili iweze kutekeleza wajibu wake kama ambavyo imepangwa. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwa kweli kama viongozi suala hili ni nyeti, leo hapa Waziri hana fedha na nilitarajia Waziri wa Fedha angekuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe kwa muda nilikuwa na matatizo ukanipeleka Wizara ya Maliasili na Utalii; Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Wajumbe walilipigia kelele suala hili na wakamtuma Mwenyekiti wa Kamati aende kwenye Kikao cha Kamati ya Uongozi pamoja na Kamati ya Bajeti na akali-*address* suala hili. Nilitarajia kuona walau wangepata hata shilingi bilioni tano kwa sababu tayari walilianza kulifanyia kazi kabla Wizara hii haijaja kwenye Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimetoka Kanda ya Ziwa, Mkoa wa Mara, kule tunafuga, tunalima, tunahifadhi, migogoro imekuwa kila siku, kweli tunakosa shilingi bilioni 10

kuipa hii Tume ya Mipango, ina watu wasomi, wenye molari, wanakosa fedha ya kwenda kuipanga nchi yao wanayoipenda ili kuondokana na migogoro ya ardhi. Kama Bunge tuwatendee haki Watanzania, tutimize wajibu wetu; na tunajua wewe una mamlaka makubwa na unaipenda nchi yako suala hili tulifanyie kazi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana, Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Esther Matiko ajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii, kwanza kabisa nasema hoja iliyotolewa na mtoa hoja ni hoja ya msingi sana na muhimu sana kwa manufaa ya Taifa. Lakini nataka nimkumbushe mtoa hoja kwamba Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi alioutaja ulipitishwa katika Bunge hili ukiletwa na Serikali; kwa hiyo, Serikali yenyewe kwanza iko *consign* na suala la kuhakikisha kuwa kuna matumizi bora ya ardhi. Kwa hiyo, tujue kwamba Serikali ndiyo mdau wa kwanza anayeona umuhimu wa kuwa na matumizi bora ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili Waziri kasimama hapa, katueleza kwamba katika fedha zilizotengwa bado wanatarajia mikopo. Tusipuuze mikopo ni sehemu ya mpango wa bajeti; hauwezi kusema mikopo siyo sehemu ya mpango wa bajeti maana hata fedha hizi ambazo leo tunazizungumza siyo kwamba zipo kwenye Hazina; tutazikusanya kutokana na kodi za wananchi ndiyo zitafanyakazi. Vivyo hivyo, mikopo tutaipata itaingia kwenye kazi zinazokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa namuomba sana Mheshimiwa Mbunge mwenzangu, dada yangu kipenzi Halima Mdee akubali kumrudishia Waziri shilingi yake, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephat Kandege atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nicholus Matiko, Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, hoja ambayo ametoa Mheshimiwa Halima Mdee ni hoja ya msingi sana. Lakini naomba nimkumbushe Mheshimiwa Halima Mdee, kwanza tunatakiwa sisi kama Bunge turidhishwe na *absorption capacity.* Katika hicho ambacho Mheshimiwa Waziri anasema kwamba anatengewa hicho ndicho tutakachoweza kumpima nacho na ni vizuri Mheshimiwa Halima akajua, kwamba kuna suala ikifika muda wa *mid-year review* tunapitia kama Bunge kuona namna ambavyo fedha imetumika na pale ambapo kuna uhitaji wa kuongeza Bunge litakuwepo.

Kwa hiyo, si vizuri tukaja tukampima Waziri katika kile ambacho amesema hiki sina uwezo wa kutumia, Tume ikatumia hiyo shilingi bilioni moja ikitumika *effectively then* tukija kama Bunge tunasema sasa katika kile ambacho tulikupa umefanya kazi hii inapimika, tukuongezee kwa sababu tunaona uhitaji upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Halima na bahati nzuri ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti naheshimu mawazo yake lakini katika *stage* hii ni vizuri aridhie na tukabaliane shilingi bilioni moja inatosha kwa kuanzia, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Nicholus Matiko atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Innocent Bashungwa ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami nimesimama kuunga hoja ya muhimu sana ya Mheshimiwa Halima James Mdee.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Wabunge wenzangu tupo hapa kwenye bajeti tunapitisha bajeti tukiamini kwamba tunachokipitisha kinakwenda kutekelezwa. Mwaka 2021/2022 tulipitisha hivi bilioni 10 lakini tumeambiwa zimetoka shilingi bilioni 1.5; bilioni 10 kwa ajili ya kupima vijiji 750, shilingi bilioni 1.5 tunaambiwa na Kamati hapa ni vijiji 100. Migogoro hii inapelekea upotevu na mauaji kwa Watanzania,

tumeshuhudia kule Mbarali na hata alikuja hapa akasoma hoja ya maelezo hapa, watu wanakatwa vichwa kwenye hivi hifadhi yaani tunaonekana ni Serikali ya ajabu kuthamini watanzania kufa kuliko kupeleka fedha ili mipango iweze kufanyika kuokoa maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko ni Mbarali hifadhi ya kule wamekuwa wakimega, waliomba kumegewa ardhi sasa hivi wanazidi kusogeza lakini tukienda kule kwetu Tarime Mkoa wa Mara, Kata ya Nyanungu tumekuwa tukipoteza vijana wetu, wakienda kule na ng'ombe wanapotelea kule, tumekuwa tukisema siku zote tusiendelee kuua Watanzania tukaacha kutenga fedha shilingi bilioni 10, sasa hivi zinatakiwa shilingi bilioni 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021/2022 shilingi bilioni tisa hatukuleka na sasa hivi tukitenge tena ina maana ni shilingi bilioni 19 hapa, tukiamua tunaweza; Serikali mkiamua kutafuta hata shilingi bilioni 40 zinapatikana ni kwa sababu hatuthamini uhai wa Watanzania na kama tunathamini uhai wa Watanzania na matumizi bora ya ardhi ni wakati sasa Serikali ilichukue hili kwa ukubwa wake zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiyi, ni maeneo mengi, tumeshuhudia hata Kibaso kwa Mara tu nazungumzia, wanakwenda wanalima barabara mpaka wanaingia kwa makazi ya watu, lakini tukitenga ikajulikana hapa ni hifadhi, hapa kwa ajili ya kilimo, hapa ni kwa ajili ya wafugaji, hapa ni kwa ajili ya kitu fulani kutakuwa hakuna miingiliano, huko Kilombero watu wanakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *valid point* na tutashangaza kabisa Watanzania watatushangaa tusipowaelekeza iende Kamati ya Bajeti fedha zipatikane. Hata tukipata fedha kama tulivyopata za Uviko zielekezwa huku tupime ardhi tena tungepeleka hata shilingi bilioni 60 siyo 19 wala tisa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya kengele imeshagonga, imeshagonga Mheshimiwa ahsante sana. Mheshimiwa Jenista Mhagama atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Mheshimiwa Selemani Jafo ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo hapa kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ardhi kwa kazi kubwa anayoifanya katika kutambua hoja zote zinazojiri katika sekta hii ya ardhi. Lakini Waheshimiwa Wabunge tumpongeze pia Mheshimiwa Rais kwa sababu mpaka sasa hivi ameshaonesha uwezo wa hali ya juu wa kutambua matatizo ya Watanzania katika sekta mbalimbali na kuyapa kipaumbele ili kutoa huduma bora kwa wananchi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa nini; Waziri wa Ardhi alipokuwa anasoma bajeti na alipokuwa anahitimisha hapa, hakuna mahala popote ambapo amesema Serikali hii Awamu ya Sita haijui umuhimu wa kupima ardhi katika nchi nzima ya Tanzania. Kwa hiyo, si sahihi kuiambia Serikali kwamba haioni *concern* ya migogoro ya ardhi katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya msingi ni nini hapa; kwa kuwa Serikali inatambua na tumekwishakusema na Waziri wa Ardhi ametoa maelezo mazuri sana, akifuatilia utaratibu mzima wa upitishaji wa bajeti ametuamia, ziko fedha zilizotengwa kwa kazi hiyo, uko utaratibu tena ni wa kibajeti kwa sababu utaratibu wa kibajeti una mapato ya ndani, una fedha za mikopo, vyote vikikusanywa pamoja utekelezaji wa bajeti unafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyeekiti, lakini Waziri wa Ardhi ametuambia kwamba pamoja na bajeti iliyotengwa fedha za mikopo lakini bado Serikali kupitia bajeti mama ya fedha tunao uwezo wa kufikiri na kuona nini lifanyike la ziada ili migogoro hii ya ardhi iweze kuondolewa kwa kuiongezea fedha Tume hiyo ya Mipango Bora ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamuunga mkono Mheshimiwa Waziri na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wale ambao wanaonesha kama vile Serikali haionji tatizo hili la migogoro ya ardhi si sahihi Serikali inatambua ndiyo maana imejipanga na ndiyo maana maelezo ya Mheshimiwa Waziri yanaonesha ni kwa namna gani Serikali itafanyakazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Bashungwa atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze kwa kusema kwamba wakati Mheshimiwa Halima Mdee anatoa hoja yake alisema kwamba Mawaziri wanazurura, Mawaziri hawazururi wanakwenda kufanya kazi. *(Makofi)*

Jambo la pili, hoja ya Mheshimiwa Halima Mdee ni hoja ambayo wote tunakubaliana kwamba ni hoja ya msingi, lakini Serikali inalitambua hili na ndiyo maana imetenga bajeti ya shilingi bilioni moja. Kama ingekuwa siyo hoja ya msingi Serikali isingetenga fedha, kwa hiyo, kitendo cha kutenga fedha ni kiashiria kwamba Serikali inatambua hii hoja ni ya msingi na hapa tunachokijadili ni kwamba hii bajeti haitoshi. Lakini suala la kwamba Serikali haioni kipaumbele katika suala la upimaji na upangaji ardhi, hiyo siyo kweli. Serikali inalipa umuhimu na uzito na ndiyo maana imetenga fedha. Kwa hiyo hoja hapa fedha iliyotengwa haitoshi hilo nilitaka niliweke sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwanza nimpongeze sana kwa bajeti makini ambayo ameiwasilisha na sisi upande wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Mheshimiwa Waziri na timu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi tupo kwenye majadiliano ya kuona zile halmashauri ambazo zinakusanya mapato ya ndani shilingi bilioni tano na kuendelea kuona uwezekano kuwa na zenyewe zinatenga kiasi cha fedha cha kuunganisha na hiki ambacho kimetengwa kwenye bajeti. Hicho ni kiashiria

kingine cha kuonesha namna gani Serikali inachukulia jambo hili kwa uzito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Waziri amesema mojawapo ya *framework* ya kupata fedha ni mkopo ametaja hapa, kama lingekuwa siyo la muhimu Serikali isingekuwa kwenye mpango wa kupata mkopo ili kuendelea na suala la upimaji na upangaji ardhi. Kwa hiyo, nimuombe dada yangu Mheshimiwa Halima Mdee, tumekuwa wote kule Ubungo Kibangu wewe ni dada yangu, naomba Mheshimiwa Waziri umpe shilingi yake ili haya tuliyoyajadili tukayatekeleza, nakuomba sana dada yangu Mheshimiwa Halima Mdee, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Hoja ya ujirani mwema jamani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Selemani Jafo atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Mtoa hoja ajiandae kuhitimisha hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula kwa kazi kubwa aliyofanya katika bajeti hii, lakini pili, nimpongeze dada yangu, Mheshimiwa Halima Mdee, kwa hoja yake ambayo ikihitaji jinsi gani kuweza kutatua matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe dada yangu Mheshimiwa Halima, jambo la kwanza namuonea huruma dada yangu, mwanamke mwenzako wa kwanza leo kutaka kushikiwa shilingi humu ndani, mimi ni hilo tu. Kwa hiyo, nimuombe tu kwanza aweze kumrudishia shilingi yake, isipokuwa jambo limesikika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kama ninavyofahamu kwamba bajeti iliyotengwa hapa lakini ninafahamu kwamba katika mpango ambao mwaka huu utakwenda kufanyika, ukiacha maeneo mengine inawezekana hatujaangalia mafungu mengine. Katika ofisi

ambayo ndugu yangu Mheshimiwa Bashungwa hapa, aliwasilisha bajeti yake katika mwaka wa fedha unaokuja kuna fedha nyingi karibu maeneo 45 katika zile mamlaka 184 kwanza yataweza kuondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo hayo yana fedha maalum kupitia *World Bank,* licha ya mipango mingine lakini kuna mipango ya utengenezaji wa mipango mbalimbali katika miji hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, katika maeneo 184 tunatoa hayo 145 ambayo yatakuwa na fedha zake maalum tofauti na Tume hii ya Mipango, ambayo Tume ya Mipango itakuwa kazi yake ni kutumia fedha hizo kutoa maelekezo katika utaratibu wa utengenezaji katika maeneo haya, hilo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninafahamu pia katika Mamlaka za Serikali zetu za Mitaa tulizonazo kuna mipango mbalimbali inaendelea katika Halmashauri mbalimbali, isipokuwa jambo kubwa ni jinsi ya kui-*integrate* pamoja, kwamba ukiangalia *total budget* katika mafungu mbalimbali ni kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hoja ni kweli ni ya msingi lakini katika utekelezaji ukiangalia *it is more than one billion* tuliyokuwa nayo hapa katika mafungu mbalimbali. Lakini kwa muktadha ule ule dada yangu Mheshimiwa Halima, hebu kwanza muachie. Halafu leo ni Ijumaa basi kwa mara nyingine. *(Kicheko)*

Wewe umesema, Serikali tumesikia, jambo letu kubwa ni kufanya haya mambo yaende vizuri kwa mustakabali wa nchi yetu. Basi shilingi hii irudi twende katika utekelezaji na mimi naamini katika *budget review* ya mwezi Desemba, inawezekana kama kuna mapungufu mengine tutaweza kuya-*address* vizuri, kwa sababu mwisho wa siku tunataka nchi yetu iende vyema. Nishukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilishamtaja Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na nikasema atafuatiwa na mtoa hoja, lakini nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Simbachawene halafu hapa nikasahau kumuorodhesha. Kwa hiyo, baada ya Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa George Boniface Simbachawe halafu mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kama walivyosema waliotangulia nieleze umuhimu wa hoja iliyotolewa, lakini nataka niweke rekodi sawa katika Bunge hili na nimuombe sana Mheshimiwa Halima Mdee aniazime sikio lake msomi mwenzangu huyu labda huenda tutaelewana na nikamshawishi arudishe shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko hoja kubwa mbili; ya kwanza si kweli kwamba hakuna pesa juu ya jambo hili kama ilivyosemwa. Pesa hizi zipo na zimekwishasainiwa na kuweka rekodi sawa nataka nikumbushe Bunge lako kwamba tarehe 21 Februari, 2022 kama kumbukumbu itakuwa nzuri, Serikali ilisaini mkataba na *World Bank* na siku hiyo ya mkataba kama mtakumbuka vizuri, kwa wale ambao tunafuatilia mitandao ya kijamii, *television* na mambo mengineyo, Wizara mbili zilisaini mkataba siku moja; ilikuwa ni Wizara ya Elimu na Wizara ya Ardhi na bahati nzuri zaidi katika mkutano huo Wizara hizi mbili ziliwasilishwa na Makatibu Wakuu wao. Kwa upande wa Wizara ya Ardhi alikuwepo ndugu yetu Bwana Kijazi, upande wa Wizara ya Elimu alikuwepo Dkt. Sedoyeka. Nataka niliweke vizuri kwa sababu iko kauli ilitolewa hapa kwamba hizo fedha zinatarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri alieleza kwamba fedha hizo zipo. Na ule mkataba umekuwa *effective* kuanzia tarehe 18 Mei, 2022. Sasa nilitaka niweke jambo hili vizuri kwa sababu haya mambo yana taratibu zake na kwamba Bunge lielewe kwamba pesa hizi zipo, hili la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo nataka nieleze kwa ruhusa yako ni kwamba katika mwaka wa fedha huu

ambao watatupitishia mafungu yetu haya dola za Kimarekani *4.9 million,* maana yake ukizungumza dola na kiingereza kidogo, dola za Kimarekani milioni 4.9 zitatumika kwa ajili ya mchakato ule wa fedha za *World Bank* kama ilivyoelekezwa na mradi huu wa vijiji ukiwemo ndani yake. Hili ni jambo ambalo lipo wazi na ndiyo mipango na ndivyo ilivyo. Jambo hilo nataka nieleze wazi na ndivyo ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo pia nataka nieleze kwamba jambo hili la vijiji ni jambo mtambuka. Kama alivyoeleza ndugu yangu Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ya kwamba kila kijiji au kila Halmashauri ni mamlaka ya upangaji. Kwa lugha nyingine maana yake hata ninyi Wabunge wenzetu humu ndani kwenye Halmashauri zenu kabla hamjaangalia fedha za *World Bank* mnatakiwa muwe mmepanga kupima vijiji hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe, siyo jambo la tume peke yake kufanya shughuli hizi. Kwa maana hata mimi kule Chalinze natakiwa sasa hivi tuwe tumeshapanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi ninalotaka nilikumbushe Bunge lako, kwa gharama ya sasa kupima kijiji kimoja ni shilingi milioni 15. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwamba kwa zile halmashauri ambazo zinakusanya mapato kuanzia shilingi bilioni tano maana yake utaratibu wa maelekezo utapelekwa. Lakini siyo jambo jipya, limekuwepo siku zote kwa sababu kule Chalinze mpaka sasa hivi tunaendelea na kupanga vijiji zaidi ya vinane ikiwa ni sehemu ya mkakati katika zile halmashauri ambazo zinapata zaidi ya shilingi bilioni tano kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI amesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka nimshawishi Mheshimiwa Mbunge apate kuelewa tu kwamba hili jambo ni mtambuka, zipo shughuli ambazo zinafanyika ndani ya Wizara kupitia Tume ambayo ni kupitia bajeti hii, lakini ni kweli kwamba kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri, bajeti bado ni ndogo, tutaongeza. Lakini nataka mfahamu kwamba ziko

hatua zinazochukuliwa ndani ya Serikali kuhakikisha kwamba bajeti hii inatimia, lakini pia kwa kushirikiana na Wizara nyinginezo ikiwemo Wizara ya TAMISEMI, jambo hili nalo linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliyopo mbele yetu ni ya kuondoa shilingi kwa ajili ya kushinikiza Serikali iweke fedha za kutosha ili kupima nchi nzima ambapo kwa kweli hata hizi shilingi bilioni 10 zinazosemwa zikitolewa tutasogea kidogo, lakini hatuwezi kumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni hoja *valid,* hakuna anayeweza kubishana kabisa na aliyetoa shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hata mtu mwingine angeweza kufanya hivyo humu ndani angekuwa yuko sawasawa tu kwa sababu ni kweli kwamba tukipima nchi yetu yote tutakuwa tumefanya jambo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niwakumbushe tu Waheshimiwa Wajumbe na mtoa hoja pia kwamba Ibara ya 74 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 inasema kwamba; "Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama cha Mapinduzi kitaendelea kuchukua hatua za kuendeleza rasilimali za ardhi kwa kutambua kuwa hiyo ni rasilimali muhimu katika uhai na ustawi wa binadamu na Taifa. Chama kitahakikisha Serikali inaweka mikakati madhubuti ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii na ustawi wa watu wote kwa kuzingatia sera, sheria, miongozo na taratibu za uendelezaji wake. Katika kipindi hicho, chama kitaelekeza Serikali kuendelea kutekeleza yafuatayo:-"

Mheshimiwa Mwenyekiti, yametajwa mazingatio muhimu ikiwa ni pamoja na kupima na kumilikisha maeneo milioni 2.5 mijini na maeneo milioni 2.6 vijijini; hii ni ilani ya miaka mitano. Kwa hiyo maelekezo haya yanakwenda *in line* tu na kile anachokisema mwenzetu Mheshimiwa Halima Mdee kwamba tutenge fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu muhimu hapa ni vingi na kama fedha ingekuwepo ya kutosha tungeweza kutoa kwenye vipaumbele vilivyopo vingi. Hili la kupima ardhi ni sawa, ni muhimu, lakini je, ni muhimu kuliko dawa? Je, ni muhimu kuliko elimu? Kwa hiyo, vipaumbele ni vingi na ndiyo maana tunachagua tuanze na hili tuache hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni suala la kupima tu yapo maeneo hapa yamepimwa, Kinondoni imepimwa, lakini leo kuna migogoro. Imepimwa na imemilikishwa lakini leo kuna migogoro. Kwa hiyo, migogoro ni tabia tu na hulka wala kupima siyo muarobaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa Naibu Waziri wa Ardhi, nafahamu kwamba tume hii ina kazi kubwa ya kufanya, inapaswa ipewe fedha, lakini pamoja na kupewa fedha zile jitihada zinazofanywa na Serikali ni kubwa na niipongeze Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwamba ina mipango mingi kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vina haki ya kupanga, mamlaka za upangaji ziko nyingi, Halmashauri zina haki ya kutenga fedha. Kwa hiyo ukijumlisha *cumulatively* unapata, pamoja na hii *one point something billion,* ukajumlisha na fedha zinazotumika kule, ni fedha nyingi inayotumika kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi rai yangu nimuombe tu Mheshimiwa Mdee, mwenye hoja kwamba aridhie shilingi ya Waziri ibaki, lakini Serikali imesikia, na tutazingatia haya ambayo yametolewa maoni ya kwake na Waheshimiwa Wajumbe wengine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe, sasa nimuite Mtoa Hoja, Mheshimiwa Halima James Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji wa mwisho ameelezea Ilani ya CCM, lakini nadhani anafahamu vilevile Mpango wa Taifa, moja kati ya nyaraka inazoangalia ni ilani ya chama ambacho kipo madarakani. Kwa hiyo, anachokisema ni sahihi na anachokisema kimekuwa *reflected* sasa kwenye mpango wa miaka mitano, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, majibu yake vilevile yanaonesha kwamba kuna changamoto ya ku-*plan.* Kwa sababu kama unajua una uwezo wa kufanya vitu kumi, kwa nini una-*plan* vitu mia? Na ndiyo maana mpango wa miaka mitano uliopita tulishindwa kufanikiwa kwa asilimia 50 kwa sababu tuli-*plan* kupitiliza uwezo wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa iko *very simple* na mimi nimeamua kuwa chawa wa Waziri, kwa sababu huyu ni mwanamke mwenzangu nataka a-*perform.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameeleza Mheshimiwa Esther Matiko hapa kwamba katika mpango wetu wa miaka mitano, mwaka wa kwanza, 2021/2022, katika kumi mlitoa moja na Kamati ya Bunge imesema, siyo mimi. Mwaka 2022/ 2023 basi mngesema siyo tu mtoe kumi, mtoe 19 na za mwaka uliopita. Wameomba shilingi bilioni 10 mnawapa shilingi bilioni 1.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi kama Bunge hapa tunachoangalia ni bajeti. Mheshimiwa Naibu Waziri ananiambia eti sijui mkopo wa *World Bank.* Mlivyosaini...

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajibu...

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza.

Ulishatoa hoja mwanzoni, ulielezea hoja yako, baadaye watu wamekuunga mkono, Waheshimiwa Wajumbe wamejadili. Kwa hiyo, sasa hivi muda wako wa kuhitimisha hoja hapa umebakiza dakika moja.

Kwa hiyo ndiyo maana nataka nikupeleke sasa elekea kule mahali shilingi unarejesha au hapana, ndiyo hicho. Kwa hiyo una dakika moja tu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najibu hoja kwa sababu ukiwa unahitimisha hoja lazima ujibu hoja *otherwise* vitu vinaweza vika-*hang.* Lakini niseme hivi kwa kuwa mimi nimeamua kuwa chawa wa Waziri, nikitoa shilingi nitakuwa namuonea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba nipate *commitment* ya ziada kwamba kwenye ile fedha ya *World Bank* itatolewa hela ambayo hapa haipo, itatolewa hela ya kumuongezea Waziri, *commitment* ya kweli. Mimi shilingi yake nairudisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana.

Sasa Waheshimiwa Wajumbe, kwa mujibu wa Kanuni zetu, kwenye ngazi hii Waziri huwa hapewi tena nafasi ya kuzungumza. Kwa hiyo, kwa sababu Mheshimiwa mwenye hoja ameshairejesha shilingi, Waziri ameshasikia hoja na pia amewasikia Waheshimiwa Wabunge walichochangia kuhusu hoja hii ambayo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaendelea, majina niliyokuwa nimeletewa kwenye mshahara wa Waziri ni hayo mawili. Sasa niwahoji kwenye kifungu hiki ambacho kina mshahara wa Waziri.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit* ... Sh. 1,536,630,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit* ... ... Sh. 966,668,000
Kifungu 1004 – *Management Information System Unit* ... ... ... ... ... ... ... Sh. 1,747,122,200
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit* ... ... ... ... ... Sh. 350,880,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 514,236,000
Kifungu 1007 – *Govt Communication Unit* ... ... Sh. 454,424,000
Kifungu 1008 – *Legal Services Unit* ... ... ... ... ... Sh. 608,328,000
Kifungu 2001 – *Land Administration Division*...Sh. 13,700,386,516
Kifungu 2002 – *Surveys and Mapping Division* ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 10,145,495,390
Kifungu 2003 – *Registration of Titles Unit* ... ... Sh. 1,215,620,000
Kifungu 2004 – *Valuation Unit* ... ... ... ... ... ... Sh. 4,116,111,000
Kifungu 2005 – *Dar es Salaam Land Office* ... Sh. 1,145,860,000
Kifungu 2007 – *Dodoma Land Office* ... ... ... ... Sh. 750,720,000
Kifungu 2008 – *Tabora Land Office* ... ... ... ... ... Sh. 676,120,000
Kifungu 2009 – *Mwanza Land Office* ... ... ... ... Sh. 833,680,000
Kifungu 2010 – *Kilimanjaro Land Office* ... ... ... Sh. 707,080,000
Kifungu 2011 – *Mtwara Land Office* ... ... ... ... Sh. 575,250,000
Kifungu 2012 – *Mbeya Land Office* ... ... ... ... ... Sh. 756,160,000
Kifungu 2013 – *Simiyu Land Office* ... ... ... ... Sh. 578,060,000
Kifungu 2014 – *Arusha Land Office* ... ... ... ... ... Sh. 695,440,000
Kifungu 2015 – *Geita Land Office* ... ... ... ... ... Sh. 571,600,000
Kifungu 2016 – *Njombe Land Office* ... ... ... ... Sh. 591,130,000
Kifungu 2017 – *Katavi Land Office* ... ... ... ... ... Sh. 552,320,000
Kifungu 2018 – *Coastal Land Office* ... ... ... ... Sh. 674,340,000
Kifungu 2019 – *Iringa Land Office* ... ... ... ... ... Sh. 557,820,000
Kifungu 2020 – *Kigoma Land Office* ... ... ... ... Sh. 621,560,000
Kifungu 2021 – *Lindi Land Office* ... ... ... ... ... ... Sh. 581,960,000
Kifungu 2022 – *Mara Land Office* ... ... ... ... ... Sh. 718,760,000
Kifungu 2023 – *Morogoro Land Office* ... ... ... ... Sh. 841,640,000
Kifungu 2024 – *Ruvuma Land Office* ... ... ... ... Sh. 647,200,000
Kifungu 2025 – *Shinyanga Land Office* ... ... ... Sh. 618,680,000
Kifungu 2026 – *Singida Land Office* ... ... ... ... Sh. 598,650,000
Kifungu 2027 – *Tanga Land Office* ... ... ... ... ... Sh. 765,400,000
Kifungu 2028 – *Kagera Land Office* ... ... ... ... ... Sh. 688,295,000
Kifungu 2029 – *Rukwa Land Office* ... ... ... ... ... Sh. 494,480,000
Kifungu 2030 – *Songwe Land Office* ... ... ... ... Sh. 542,060,000
Kifungu 2031 – *Manyara Land Office* ... ... ... ... Sh. 610,960,000

Kifungu 3001 – *Rural and Town Planning Division*... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 8,722,309,000
Kifungu 3003 – *District Land and Housing Tribunal Unit* ... ... ... ... ... ... ...Sh. 5,775,937,600

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamatiya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 03 – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

Kifungu 1001 – *Directorate of Corporate Services*... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 1,574,193,000
Kifungu 1003 – *Procurement and Management Unit* ... ... ... ... Sh. 138,295,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit* ... ... ... ... ... Sh. 128,780,000
Kifungu 1005 – *Legal Services Unit* ... ... ... ... ... Sh. 232,070,000
Kifungu 2001 – *Directorate of Land Use Planning, Management & Coordation Division* ... ... ... ...Sh. 662,539,000
Kifungu 2002 – *Directorate of Research, Compliance & Information* ... Sh. 615,787,000
Kifungu 2003 – *Zonal Offices* ... ... ... ... ... ... ... Sh. 106,040,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamatiya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*... ....Sh. 500,000,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning* Unit... ... ... Sh. 970,000,000

Kifungu 2001 – *Land Administration Division*… … … … … ... ... ... ...Sh.15,815,572,000
Kifungu 2002 – *Surveys and Mapping Division*... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 9,867,750,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 03 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

Kifungu 1001 – *Directorate of Corporate Services*... ... ... ... … … … … … Sh.103,000,000
Kifungu 2001 – *Directorate of Land Use Planning, Management & Coordination Division*… … … … … ... ... ... ...Sh. 1,215,000,000
Kifungu 2002 – *Directorate of Research, Compliance & Information*… ... ... … … … … Sh. 92,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kuwa, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge Linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa Hoja, Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote chini ya Wizara hii kwa kupitishiwa Makadirio yao ya Mapato na Matumizi na Bunge hili na mjadala ulikuwa mzito, lakini pia mwepesi kwa yale ambayo Serikali imeshafika mahali imefanya vizuri na Wabunge wamepongeza kwamba michango katika bajeti ya Wizara hii majina yamepungua kidogo kwa kuonesha kwamba, Serikali inafanya kazi nzuri kuhakikisha wanamaliza migogoro ya wananchi kwa sehemu kubwa. *(Makofi)*

Kuna migogoro itakuwa inaendelea kuibuka, haimaanishi Serikali haifanyi kazi, lakini kwa ujumla wake mmefanya kazi nzuri na tunawapongeza sana, lakini sehemu ambazo bado kuna changamoto Waheshimiwa Wabunge hapa wengine wamesimama wametaja maeneo yao ambayo yana changamoto mmeyasikia. Na kwa namna Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Utalii inavyofanya kazi vizuri na inavyowapa ushirikiano vizuri tunaamini mtaendelea kusikiliza mawazo ya Waheshimiwa Wabunge na hata wale ambao hawakupata fursa ya kuzungumza hapa Bungeni tunaamini mawazo yao wakiwafuata mtayafanyia kazi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawatakia kila la heri katika haya makadirio ya mapato na matumizi ambayo Bunge hili limewapitishia leo. Tunawatakia kila la heri kwenye utekelezaji wa zile ahadi mlizozisema hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kwa kusema hayo, nitangaze sasa rasmi kwamba, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yamepitishwa rasmi. *(Makofi)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kuna jambo ambalo limejitokeza katika michango yetu na mojawapo ya hayo mambo linatuhusu sisi, kama Bunge. Upande wa Wizara ya Ardhi, sawa mmelichukua, lakini kwa sababu utekelezaji wake unahitaji fedha, jambo la kuongeza maeneo kwa ajili ya Bunge yale ambayo yanalizunguka Bunge, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti yuko pale naelekeza jambo hilo lielekee Kamati ya Bajeti ili mkaangalie namna ya kulifanyia kazi, ili Wizara ifanye kwa sehemu yake, Bunge lifanye kwa sehemu yake na baadaye maeneo hayo yaweze kutuweka katika hali ya usalama sisi wote kama Wabunge, lakini pia wananchi ambao hili ni Bunge lao na wanakuja kulitembelea Bunge, basi na wao wawe katika hali ya usalama. Kwa hiyo, Kamati ya Bajeti itafanya shughuli yake kwenye hoja hii. *(Makofi)*

Hoja nyingine iliyozungumzwa kwa nguvu sana, lakini yenyewe haitaelekea kwenye Kamati ya Bajeti kwa sababu tumepata nafasi ya kupata ufafanuzi kwa upande wa Serikali namna walivyojipanga na namna ya kulifanyia kazi ni hili la Tume yetu kwa ajili ya Mipango ya Ardhi. *(Makofi)*

Limesemwa na Waheshimiwa Wabunge kwa uzito, lakini pia Serikali mmetoa majibu. Tunaamini katika kipindi hiki mtaendelea kulifanyia kazi ili maeneo, hasa yale yenye migogoro basi yaweze kufanyiwa kazi kwa haraka zaidi halafu tufike mahali ambapo nchi yetu itakuwa yote imepimwa kwa kadri ya ahadi ya ilani, lakini pia kwa kadiri ya mpango wetu sisi kama nchi ya Tanzania. Kwa hiyo, tunaamini mtalichukua kwa uzito huo ambao Waheshimiwa Wabunge wamelieleza hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nadhani sote tumeielewa Serikali, lakini pia nyote mmelewa kwa nini haielekei kwenye Kamati ya Bajeti kwa sababu hoja sio fedha peke yake. Nadhani tumesoma ile Taarifa ya Kamati yetu ya Bunge, imeelezea changamoto ni nyingi kuliko fedha peke yake za upimaji. Wameeleza kuhusu watumishi, wameeleza mambo mengi, kwa hiyo, hayo yote lazima yafanyiwe kazi ili tuweze kufika mahali ambapo tutaona tija ya kazi wanayoifanya, lakini pia tutaona tuasonga mbele kama Taifa kwa sababu unaweza ukasema upeleke tu fedha, halafu watumishi hawapo, itafika muda hapa wa kutazama ule mwezi wa kwanza, kutazama wamefikia wapi wanasema hatuna watumishi ndio maana tumefika hapa. Kwa hiyo, Serikali iyachukue haya yote yanayoihusu Tume hii na kuweza kuyafanyia kazi kadiri mlivyoahidi hapa kwenye michango ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa bajeti yetu hii ambayo ilikuwa inajadiliwa kwa siku mbili na baada ya kusema hayo niwatakie kila la heri na ninaahirisha Bunge mpaka siku ya Jumatatu, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 06.30 mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 30 Mei, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*